# *Ishara Kuu*

Asanteni. [Ndugu mmoja anasema, "Nasi tunataka kukualika urudi, amina, yapata mwaka mmoja tangu sasa, wakati wowote. Amina."—Mh.] Asanteni. Asanteni sana. Mungu awabariki. Asanteni. Asanteni, sana. Jamani, hilo hakika linanifanya nijisikie kukaribishwa. Asanteni sana. Ninathamini hilo.

2 Na wakati mwingine wahudumu, mwajua, tunapoweka jitihada zote tuwezazo moja kwa moja katika jambo lolote, kisha tuone linathaminiwa na watu, jamani, hilo linakufanya tu ujisikie vizuri sana. Hakika ninawathamini, daima nitakuwa nikiwaombea. Na Bwana akipenda, nitarudi tena. Nami ningetaka kurudi na kuona . . . [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Kama akikawia na ni mapenzi Yake, tutarudi kuwaona tena.

3 Hii ni, ninaamini, yapata safari yangu ya tatu hapa kwa vyovyote vile. Na kwa hiyo tulikuwa tumetumainia kurudi wakati tunaweza kukaa labda muda mrefu zaidi kidogo, tupate uwanja, na kadhalika, kwa muda mrefu zaidi kidogo na . . . [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Imekuwa ni fu—furaha kuu, mmoja wa mikutano mizuri sana ambayo tumekuwa nayo katika muda mrefu sana, sana, ushirika mzuri sana, ushirikiano, upendo. Hicho ndicho kitu kinachoyeyusha mioyo ya watu pamoja, ni upendo wa Mungu.

4 Na yote nijuayo, na ningeninii . . . Kama ningekuwa na karama zote za Mungu katika mahali pakubwa ambapo ningeweza kuingia na kupokea zawadi yoyote niliyotaka, ningekubali upendo juu ya yoyote ya hizo. Afadhali niwe na upendo kuliko karama zote alizo nazo Mungu, kwa sababu "zilipo lugha, zitakoma; palipo na unabii, utabatilika," bali ukiwa ni upendo, unadumu milele, nami . . . upendo.

5 Nafikiri tu hilo ndilo neno kuu kuliko yote, *upendo*. Linagawanywa katika maneno mawili mbalimbali. Kuna u—upendo unaoitwa upendo wa *fileo*, huo ndio upendo tulio nao sisi kwa sisi, wa kawaida. Halafu kuna upendo wa *Agapao*, unaotoka kwa Mungu, hizo ni heshima za kiungu na upendo. Nami nina furaha sana kuwa hapa katika ushirika huu alasiri ya leo ambapo awamu zote mbili za upendo zinatenda kazi, tukishirikiana sisi kwa sisi, na upendo wa Mungu uliomiminwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu.

6 Ninataka kuishukuru kwaya hiyo ndogo. Naye Ndugu Borders ndio kwanza aje na kuniambia, kasema, "Ndugu Branham, hiyo si kwaya iliyoteuliwa, hao ni watu tu wa uamsho huu, watu mbalimbali tu." Mnapaswa kupata jina la mmoja

na mwenzake na kuunda kwaya, hiyo ni nzuri kweli. Na bila shaka ninaupenda ujumbe wenu pia, kwamba mmezaliwa mara ya pili. Nina furaha kushiriki pamoja nanyi katika jambo hilo, nimezaliwa mara ya pili pia kwa Roho yeye yule na katika familia ile ile, nawe ni ndugu yangu na dada kwa hilo.

7 Hapo ndipo mahali pekee ambapo ushirika huo unaweza kuwapo, ni chini ya Damu ya Yesu Kristo. Mungu akifanya uamuzi, hauna budi uwe hivyo milele. Nao uamuzi wa kwanza wa Mungu wa kuwaleta watu katika ushirika pamoja naye Mwenyewe ulikuwa ni chini ya damu, tangu bustani ya Edeni hata dakika ii hii, hapo ndipo mahali pekee ambapo Agano la Kale, mahali pamoja tu, palipokuwa chini ya damu. Ayubu, jinsi alivyosimama imara juu ya hilo, akijua walipomwita mwenye dhambi kisiri, hata hivyo alijua alikuwa chini ya damu iliyomwagika, na kila kitu ilibidi kiwe sawa. Kwa hiyo tuna furaha kwa ajili ya jambo hilo leo.

8 Sijui tu jinsi ya kutoa shukrani zangu kwa ajili ya hawa ndugu wazuri hapa, ninyi ndugu. Jinsi mmekuwa wazuri, sijawahi kuwa na udhamini mzuri zaidi maishani mwangu, mmekuwa tu watu mashuhuri katika kila kitu. Ninatumaini ya kwamba Mungu atawasha moto wa uamsho katika kila moja ya makanisa yenu hiyo ita—itaninii tu, itawabidi kujenga makanisa makubwa zaidi, na kupanuka, na kuvuta mahema yenu, na kupanuka zaidi, na kuendelea tu moja kwa moja. Pia jalia mioto ya uamsho isiishe mpaka tutakapomwona Yesu uso kwa uso.

9 Hakujakuwako na kitu ambacho tumeomba ama chochote kile, pasipo kundi hili la watu kuwa tu likisaidia kikamilifu kwa kila njia wawezayo, wakiketi hapa jukwaani, wakiwakilisha Ujumbe. Na, mwajua, kila mmoja wetu huenda akawa na jambo fulani dogo *hapa* ama *pale* ambalo huenda tusikubaliane sisi kwa sisi, kamwe hakuna neno moja lililosemwa, lolote lile tu, tunalichukua na kuendelea moja kwa moja. Sasa, huo ndio mnaouita ushirika, hiyo ni kweli, ushirika halisi.

10 Mungu awabariki, ndugu zangu. Usiku kamwe hauingii giza kupita kiasi, ama mvua kunyesha sana, ila ambayo mimi ningefanya chochote niwezacho, kuwaombea wakati wote. Niombeeni, ninajiandaa kuingia kwenye huduma fulani za kimishenari, na mahali pagumu, nitakuwa nikitegemea, nina kundi la ndugu hapa wanaoniombea. Mnaona?

11 Natumaini kurudi pamoja nanyi tena hivi karibuni, wakati mwingine ambapo tunaweza kukaa muda mrefu zaidi, na—na kuwa tu na wakati ambapo haitatubidi kuharakisha kuingia, na kuruka nje, na kuruka ndani namna hiyo. Hilo humtia kila mtu wasiwasi, nalo, watu wanaoombewa, linawatia wasiwasi. Yapata tu wakati wanaanza kujaribu kuelewa nusu kile unachotaka kusema, ndipo inakubidi kuondoka, unaona, nao hawalipati.

12 Lakini hebu niwaambie hili: Ikiwa nimepata neema machoni penu, kutakuwako na watu wengi, wengi sana watakaokuja hapa waliokuwa wagonjwa, labda hawatajua jambo hilo wakati huu, bali angalieni mwone katika makanisa yenu na kadhalika, ndugu, kumekuwa na ninii. . .mambo mengi sana yaliyotukia hapa hata nisingeweza kuwaita kwenye kusanyiko namna hiyo, upesi tu kadiri liwezavyo kutendeka. Nami nisingeweza kufanya hivyo, ndipo nikawazia, "Vema, mradi tu wawili au watatu, ama wanne, watano, sita, wowote wale, walizungumziwa, hao wengine wangeelewa." Kumekuwa na imani nzuri huko nje, na imani hapa, kila mahali pamekuwa na imani nzuri, ninaithamini.

13 Na kuninii. . .Nina baadhi ya ndugu zangu hapa ambao sijawahi kuwaona bado mkutanoni, niliwaona huko kwenye kanisa la. . . sinagogi hivi majuzi. Ndugu Fred Sothmann, mmoja wa wadhamini wetu kutoka kanisani, Ndugu Fred, uko hapa? Simama, kama upo. Ndugu Fred Sothmann, huko nyuma kabisa kuelekea nyuma kule, yeye na mke wake na familia.

14 Nami nasikia ya kwamba Ndugu Tom Simpson yupo hapa pia, marafiki wa Canada wanaokaa pamoja nasi Jeffersonville. Mko wapi, Ndugu Tom na familia yake? Ndugu Tom pia amerudi, sasa kutoka hapa kwenda nje kwa namna fulani ni vigumu, nuru inaangazia upande *ule* kule, siwezi kuona.

15 Ndugu Banks Wood, ndugu mzuri ambaye alikuwa ni Shahidi wa Yehova, naye akaja kwenye mmoja wa hiyo mikutano, naye akaona jinsi Bwana alivyokuwa akifanya kazi. Na mwanamke, ama, msichana aliyekuwa na huu hapa. . .alikuwa akigeuka kuwa jiwe miguuni na mikononi mwake, asingeweza kuisogeza, ilikuwa tu imekakamaa. Nasi tukamwombea, Roho Mtakatifu akaja usiku mmoja, na kulitamka, kisha akamwambia, "BWANA ASEMA HIVI, utakuwa mzima." Ndipo kesho yake asubuhi, alikuwa amekimbia juu chini kwenye vipandio vitatu au vinne vya ngazi, kisha akaingia jengoni akimsifu Mungu kesho yake. Sasa, hilo lilimshangaza sana.

16 Kwa hiyo alikuwa na mvulana, David, jamaa mdogo, alikuwa na polio, mguu uliokunjamana chini yake. Nilitoka kwenye mkutano huo nikaenda Uswidi, Uswisi, ama, Uswidi, naamini ndiko, na Norwe. Ndipo niliporudi nilikuwa na mkutano huko juu kwenye. . . katika Ohio ya juu kule, ninasahau jina la mahali hapo, karibu na yale Maziwa Makuu.

17 Ndipo usiku mmoja, nilipokuwa nikizungumza, na umati mkubwa wa watu, ndipo nikamwona mvulana mdogo aliyevaa koti la manjano, alikuwa na mguu mmoja uliokunjamana, akichechemaa alipokuwa akijaribu kutembea. Ndipo Roho Mtakatifu akamgeukia Banks Wood, huko chini kabisa kutoka LaGrange, Kentucky, akiwa na m—mvulana mdogo

aliyelemaa, naye Bwana angemponya, alikuwa anaenda kuponywa. Haikumbidi kungojea, papo hapo mguu huo uliolemaa ukanyooka.

18 Ndugu Wood yupo hapa leo mahali fulani. Sijamwona tangu wakati huo, lakini ninajua yuko hapa, yeye ndiye mwuza vitabu. Mwanawe, mvulana huyo mwenye mguu uliolemaa, ni vigumu kwake, inambidi kusimama, aangalie wakati mwingine ulikuwa ni mguu gani, ulioponywa. Ameoa na ana watoto wawili wazuri, yeye na mke wake wako pamoja nasi leo.

19 David, uko mahali fulani, humu jengoni? Waweza kusimama? Kama ningeweza kuona, mimi. . . ni yeye. . . David, naam, huyo hapo. Huyo hapo shahidi wa nguvu za Mungu, David Wood, mvulana aliyelemazwa na polio, na sasa anaishi kama kawaida tu, na mguu wake ni mkamilifu tu kama ule. . . uwezavyo kuwa. Neema ya Mungu!

20 Ndugu Wood, Ndugu Banks Wood, na Dada Wood, wao ni. . . mnajua walilofanya? Yeye ni mkandarasi, na mzuri pia, mjenzi, amekuja kutoka kwenye shule ya wakandarasi na wajenzi. Lakini alipofanya hivyo, aliongoka, nikambatiza, akampokea Roho Mtakatifu.

21 Halafu basi, bila shaka watu wake wakiwa ni Mashahidi wa Yehova, mara walikuwa wakitaka kumtenga, sasa hivi. Kwa hiyo ndugu yake akashuka akaja kuzungumza naye, naye alitaka kujua mahali huyu "mhubiri tapeli" alipokuwa ambaye alikuwa akikimbia na kujipumbaza naye.

22 Naye Bw. Wood akauza kila kitu alichokuwa nacho, akapangisha nyumba zake, kisha akahamia kule, naye ni jirani yangu, mahali pote, jirani aliye karibu sana. Nami nawaambia, nina furaha ninaweza kusema hivi kuhusu Ndugu Wood alasiri ya leo: yeye ni Mkristo wa Matendo 2, mwanaume halisi.

23 Ndipo ndugu yake akashuka kuzungumza naye. Nao walikuwa. . . Baba yake alikuwa msomaji katika Mashahidi wa Yehova na mtu mzuri. Nami sikuwa nimewahi kumwona yeyote wa watu wake. Kwa hiyo ndugu yake akashuka kuja kuzungumza naye, naye akashangaa huyo "mhubiri bandia" alikuwa wapi.

Kasema, "Yuko *huko* nje akikata nyasi, uani."

24 Nikaja na kofia ya kale iliyochanika, nikaketi chini na kuzungumza naye, ndipo Roho Mtakatifu akashuka na kusema, "Wewe ni—wewe ni mtu aliyeoa, umemwacha mke wako, una wavulana wawili wadogo."

Ndipo akamtazama Ndugu Wood kule nyuma, kana kwamba kusema, "Naam, ulimwambia hivyo."

25 Nikasema, "Ninajua ulichosema. Lakini kamwe hakukwambia hivi: Unazurura na mwanamke, naye ana nywele za kahawia. Pia, siku chache zilizopita usiku ulikuwa

umesimama mlangoni, mtu fulani alibisha mlango na ni jambo zuri hukuenda ulipoangalia dirishani, maana huyo mtu angeninii, angekupiga risasi kichwani kwa bastola." Hilo lilitosha. Ndipo nikambatiza, akapokea Roho Mtakatifu.

26 Ndipo akashuka dada, mwanamke mrembo, akashuka, alitaka kuona hayo yote yalihusu nini. Nikambatiza, akampokea Roho Mtakatifu. Ndipo baba akakasirika sana, naye akashuka. Kweli, alikuwa ashuke ati na kuninyosha sawasawa, maana ati nilikuwa nimekosea kabisa katika Fundisho langu.

Ndugu Wood akasema, "Hebu tumpeleke tu kuvua samaki."

27 Nikasema, "Vema." Kwa hiyo tukaanza kushuka kwenda Kentucky, kuvua samaki. Nilikuwa tu nimwache aongee. Hiyo ndiyo njia bora zaidi, mwajua, kuwaacha wataje ki—kitu chenyewe.

28 Kwa hiyo asubuhi hiyo, ilinyesha usiku kucha, na kesho yake asubuhi tulipovuka Mto Ohio, nilisema, "Vema sasa, vijito vyote. . . " Ono likatokea, nikasema, "Vijito vyote vitajaa matope. Hatutaweza kuvua samaki mpaka tutakapofika mahali hapa tunapoenda," yapata maili mia moja. "Halafu basi, kutakuwa kuzuri sana na shwari, nasi tutavua samaki, mvua ilikwepa tu, kwa hiyo tungeweza kuvua samaki. Halafu basi, tunaenda, leo, hatutashika chochote."

29 "Na usiku wa leo, kuelekea usiku, Bw. Banks Wood, hapa, atamkamata samaki mdogo, kambare, nami nitashika msururu mzima wa hao. Utatumia chambo kile kile, karibu kabisa nami, nami nitakuwa na msururu mzima. Halafu basi, tutaingia yapata saa tano. Kesho yake asubuhi tutatoka, nami nitashika samaki mkubwa mwenye magamba juu yake, siwezi kabisa kuona tu ni wa aina gani, bali atakuwa ni samaki mkubwa. Hakuna wengine watakaokamatwa siku nzima."

30 Nilimwona Bw. Wood, Babu Wood, akiangalia pande zote namna hiyo, na *kusema*, kana kwamba kusema, "Loo, *naam*, tutaona jinsi hilo litakavyotokea."

31 Kwa hiyo tulipokuwa njiani tukienda tukamwambia, naye Banks alikuwa amemwambia jinsi yale maono (Na tukiwa huko nje, mimi na Ndugu Banks tunaishi pamoja, tunalala pamoja, sisi ni ndugu tu.), na jinsi ambavyo alikuwa ameona huko juu mtoni, naye Lyle alikuwa pamoja naye, jinsi, nikivua samaki alasiri moja, nilisema, "Jambo fulani liko karibu kutukia. Kutakuwa na ufufuo wa uhai."

32 Basi kesho yake asubuhi tulikuwa tukiwashika mashavu bluu kuwaweka kwenye nyugwe za kuvulia, naye Bw. Lyle, nduguye Bank, akamshika mmoja, akameza ndoana hiyo ndani kabisa. Hakuipindua upesi vya kutosha, naye akamvuta kwa nguvu akamtoa majini, na kuyavuta tu matumbo, na mashavu kutoka kooni mwake, akamtupa juu ya maji, kasema, "Ewe jamaa mdogo, umepumua ya mwisho." Naye akayumbayumba

kidogo, akakaa pale na kukakamaa, maskini samaki mdogo, ninii, mnayemwita hapa, brimu, nadhani. Naye akaelea juu ya maji kwa karibu nusu saa, kisha akaelea akaingia kwenye mayungiyungi ya di—di—dimbwini na kadhalika.

33 Nami nilikuwa nimesimama pale nikivua samaki, kando ya mtumbwi namna *hiyo*, mara kitu Fulani kikashuka kupitia kwenye miti hiyo, kikingurumia kote, wao wakakisikia, bali hawakukiona. Ilikuwa ni ile Nuru ikizungukazunguka pale, kasema, "Simama, nena na huyo samaki mdogo, naye atarejeshewa uhai wake tena."

34 Nikaitisha usikivu wa hao ndugu. Nikasema, "Ewe samaki mdogo, katika Jina la Yesu Kristo, ninakupa uhai wako." Maskini samaki huyo akageuka, akaogelea moja kwa moja mtoni upesi alivyoweza, namna *hiyo*, kisha . . . Hilo linaonekana la kubuni, bali hili *hapa* Neno la Mungu, naye Mungu ndiye Hakimu wangu.

35 Na—na kwa hiyo Ndugu Lyle alianguka tu, katika hiyo mashua, akasema, "Hiyo ilikuwa kwa ajili yangu mimi, Ndugu Branham." Yeye alikuwa ndio kwanza aokoke na kujazwa na Roho Mtakatifu kitambo kidogo tu. Naye akasema, "Hiyo ilinihusu mimi." Kasema, "Hamna lingine," kasema, "kwa sababu nilimwambia samaki huyo mdogo, 'Umepumua ya mwisho.'"

Nikasema, "La, ilikuwa tu ni Uwepo Wake."

Ndugu Banks, huko nyuma, akasimama, kasema, "'Ni vizuri kuwa hapa. Na tujenge vibanda vitatu.'"

36 Loo, na siku hiyo baadaye, yale hasa aliyoambiwa Babu Wood, yalitukia kikamilifu kabisa, vile vile, samaki yule yule, idadi ile ile kabisa, kesho yake tulipoondoka, nilisema, "Unaonaje, Bw. Wood?"

Akasema, "Vema, ni vizuri sana wakati mtu anaweza kuona samaki kabla hajawashika."

37 Kwa hiyo nikasema, "Vipi kuhusu hilo?" Sasa, nilimwongoza kwa Kristo, nikambatiza yeye na mke wake. Familia yake yote sasa imebatizwa katika Bwana, na kujazwa na Roho Mtakatifu, na wanaishi maisha ya ushindi. Hiyo ni neema ya ajabu.

38 Ndugu Wood, uko hapa? Uko wapi Ndugu Wood, Dada Wood? Uko humu jengoni? Simama, ikiwa upo. Pale, siwezi kuwaona. Mtu yeyote anayeangalia nyuma anaweza kuwaona? Loo, naam, moja kwa moja huko nyuma. Vema, Ndugu Wood, hilo ni sawa.

39 Vema, hebu tuone. Vema, sitakuwa na muda mwingi zaidi. Wengi zaidi wa marafiki zangu, Ndugu Gene Norman, ndugu mpendwa. Jinsi ningetaka kusimulia mambo fulani yaliyotukia kule! Aliondoka akahamia Tucson. Nilikuwa pamoja naye hivi majuzi kwenye safari ya kuwinda. Laiti ningaliwafanya Ndugu Fred, na hao wengine, washuhudie mambo haya! Mbona, hii . . .

tulipokuwa kwenye ile safari ndogo ya siku tatu ya kuwinda, mengi zaidi yalitukia kuelekea Ufalme wa Mungu kuliko vile ungeweza kuchukua historia tangu wakati wa Martin Luther hadi wakati huu. Hiyo ni kweli.

Ndugu Fred akasema, "Ni jambo zuri jinsi gani!"

40 Ndugu Norman, wewe na Dada Norman mko humu jengoni? Mko wapi? La—laiti mngalisimama, kama mpo. Huyo hapo. Naam, bwana. Mlisikia neno hilo, *über alles?* Huyo Mholanzi, mwajua. Wewe. . .Ni wangapi wanaojua maana ya *über alles?* "Juu ya yote, juu ya yote." Vema. Hiyo ni kweli.

41 Vema, kuna. . .Nina furaha kuwa hapa pamoja nanyi watu. Mungu awabariki. Nilisikia tu dakika chache zilizopita, nilipokuwa nikizungumza na Billy huko nje, gharama zote zililipwa. Asanteni nyote. Bwana awabariki. Nilimwambia meneja sikuzote, Bw. Borders hapa, wakati wowote, kamwe usiwaminye watu, kama gharama hazitatosha, nitaitisha nyumbani kwa kanisa langu mwenyewe mahali fulani, tutazipata. Mnaona? Nasi kamwe hatutaki kuminya, kusukuma, ama chochote kile.

42 Ndipo Billy ananiambia ya kwamba walichukua sadaka kwa ajili yangu. Asanteni, Mungu awabariki. Sikuja kwa kusudi hilo, enyi marafiki, nimekuja hapa kujaribu kuwasaidia. Lakini ninyi mkishiriki riziki zenu pamoja nami, nitafanya kila niwezalo, kwa neema ya Mungu, kuona ya kwamba zinaenda kwa Ufalme wa Mungu, kila njia niwezayo. Ninatumaini ya kwamba Mungu atawajengea makazi Ng'ambo ya pili, kusikopatikana na mauti, ambayo kamwe hayatafifia, kamwe, kamwe hakuhitaji kufanyiwa ukarabati.

43 Mpaka tutakapokutana huko Ng'ambo ya pili, kumbukeni, mimi daima ni ndugu yenu, nikijaribu kufanya lolote niwezalo kwa ajili yenu. Niandikieni, kama ninaweza kuwatumia kitambaa cha maombi, kitu fulani nilichoombea, ningefurahi kufanya hivyo.

44 Sasa, inapofikia kuuliza maswali, ni bora zaidi muwaulize wachungaji wenu, daima ninaliacha hivyo, maana, mwajua, ni bora kuwauliza wachungaji. Lakini kama ninaweza kuwasaidia kwa njia yoyote kwa upande wa kuwaombea, ama kuwafanyia jambo lolote, niandikieni. Sijaribu kupata anwani yako, kwa sababu mimi. . .Ninajaribu kumpata mtu fulani, anisaidie kujibu barua.

45 Sina mipango yoyote ya kuunga mkono, hakuna kitu hata kidogo. Vitabu hivyo huko nyuma, si vyangu, Bw. Wood amenunua vitabu hivyo mwenyewe kutoka kwa Ndugu Gordon Lindsay, na sehemu nyingi, naye huvileta tu kwa ajili ya watu, kwa ajili ya watu tu. Hatupati hata senti moja kutoka kwake, hatuchukui chochote.

46 Mkwe wa Ndugu Fred Sothmann anauza kanda. Ameshusha bei sana hata anaweza *tu* kuzitengeneza, hivyo tu. Na kwa hiyo wanazo kanda, ama chochote kile kama tunaweza kuwasaidia, tuko hapa kuwasaidia, chochote tuwezacho kufanya. Mungu awabariki.

47 Nami ninaomba maombi yenu kwa ajili yangu, popote niendapo. Na kama sitakutana nanyi tena. . . Sasa, najua kama nikirudi mwaka mmoja tangu sasa, kuna wengine, kama nikiishi kwa mwaka mwingine, naye Yesu akikawia, kuna wengine hapa alasiri ya leo hawatakuwa hapa wakati huo, mnaondoka, huu ndio wakati wetu wa mwisho kukutana. Lakini nitakapokutana nanyi Ng'ambo ya pili, ambapo sote tutafufuka katika kizazi hiki, ningali nitakuwa na hadithi ile ile, kwa neema ya Mungu. Hiyo ni kweli.

> Neema ya ajabu! jinsi hiyo sauti ilivyo tamu,
> Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, na sasa nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, lakini sasa ninaona.

48 Mungu awapende, na awabariki. Pia kumbukeni, wakati pepo zinapovuma kwa nguvu, usiku una giza na dhoruba, na wachawi kila upande, na kukupa changamoto kwake, nitakuwa nikikumbuka ya kwamba nina watu hapa juu kwenye Pwani ya Magharibi wanaoniombea.

49 Kuna joto sana alasiri ya leo kwangu kuhubiri yale niliyokuwa nihubiri, kwa hiyo Billy aliniambia huko nje, kasema, "Baba, ni afadhali," kasema, "uliahidi kuchukua kadi hizo zote za maombi," kasema, "ingekuwa afadhali kwako kuingia tu mle, na—na—na kuwashukuru watu, na—na kutoka nje." Lakini ningejisikia kama msaliti kwa Kristo, kama sikusoma Maandiko, na kusema jambo, hiyo ni kweli.

50 Nasi tutawaombea wa—wagonjwa pia, kila kadi ya maombi. Sasa, ninaomba tu kama mngeninii, iweni tu na kicho iwezekanavyo, nami nitaharakisha moja kwa moja. Ni jambo la ajabu kwamba mkutano huu ulitokea, jinsi ulivyokuja kutukia, bali Bwana aliufanya kutimia.

51 Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumwendee Mwandishi wa Neno, Bwana Yesu, kwa njia ya maombi.

52 Baba yetu wa Neema, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya wema Wako na rehema Zako. Wewe ni Mungu, tangu milele hata milele, Wewe ni Mungu. Na, Bwana, mkutano huu mdogo hapa chini pamoja na watu hawa wazuri, watumishi Wako, hawa watu wazuri huko nje ambao wameingia mifukoni mwao ku—kudhamini mkutano huu, na kulipia kwa riziki yao, ninaomba, Mungu, ya kwamba kama mkate juu ya maji, itarudi.

53 Ninawaombea hawa wahudumu, makanisa yao, watu wao, Mungu, jalia makanisa yao madogo yakue mpaka

yatakapopanuka, na jalia kutoka katika makanisa yao watoke wainjilisti wenye nguvu na wamishenari waende kote ulimwenguni. Jalia tufanye kazi, Bwana, kwa kuwa tunajua hatuna wakati mwingi zaidi wa kufanya kazi, tunaona wakati ukimalizika.

54 Hivi karibuni tunamtazamia Malaika atakayeweka mguu wake juu ya nchi na juu ya bahari, na kuinua mkono wake na kuapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, hapatakuwa na wakati baada ya haya. Alisema wakati huo siri ya Mungu itatimizwa.

55 Tunafahamu sasa, Baba, ya kwamba siri ya Mungu yenye sehemu tatu imefunuliwa kwetu. Nasi tunafahamu, na tunatazamia sasa zile Ngurumo za siri zilizotoka Mbinguni, katika Kitabu cha Ufunuo, zilizotiwa muhuri nyuma ya kile Kitabu.

56 Tufunulie, Ee Bwana, mambo tunayohitaji kwa ajili ya vita vilivyo mbele yetu. Tusamehe dhambi zetu, mambo ye—yetu mengi ya kupuuza, uovu wetu. Tunaomba, Mungu, ya kwamba, alasiri ya leo, ya kwamba utafanya mambo mengi makuu mno kuliko yote tuwezayo kufanya ama kuwazia.

57 Sasa, Baba, hatuko hapa tupate kuonekana, watu hawa hawako hapa wapate kuonekana. Kuna joto, wameketi wamevua makoti yao, wanaume, dada wa thamani wameketi hapo wakijipepea, wako hapa kwa sababu wana njaa, wanakupenda Wewe.

58 Na, Bwana, niko hapa nikiwa na koo linalokwaruza kutokana na mchanganyiko huu wa ukungu na moshi. Nami ni—ni—nipo hapa kwa sababu ninaamini ya kwamba ulikusudia kwamba tunapaswa kuwa hapa alasiri ya leo. Nao moyo wangu uko wazi kabisa, wao umefunguka kabisa, kwa hiyo ingia ndani, Bwana Yesu, na kutwambia mambo ambayo ungetaka tujue. Kwa kuwa tunaomba hayo, katika Jina la Yesu. Amina.

59 Ninataka kutangaza somo dogo ninalotaka kutumia, nataka kuliita *Ishara Kuu*. Nami nilitangaza somo langu kabla sijasoma Maandiko yangu, na hilo kidogo si kawaida. Kwa kawaida unasoma Maandiko yako, ndipo unapata somo lako, lakini unajua, wakati mwingine Mungu hufanya mambo kwa njia zisizo za kawaida, nyakati zisizo za kawaida.

60 Katika Isaya, mlango wa 7 na kifungu cha 14, ningetaka kusoma sehemu ya Maandiko, kifungu hiki kimoja, kufanya muktadha ambao nimetoa somo hili kwake.

> *Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara; Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.*

61 Tunaishi katika siku za *kuu*. Kama si kuu, haipiti. Kila kitu hakina budi kuwa ni *kikuu*, ni siku kuu. Unaenda dukani,

maskini yule mwenye duka dogo pembeni hana biashara, inawabidi kwenda kwenye supamaketi. Unapata stempu kadhaa na kuzilipia hela nyingi zaidi, yapata nikeli kwa kila moja, ati kwa maana ni supamaketi, hawawezi kukupa hizo stempu, unajua. Lakini ni—ni supamaketi, imetiwa kiyoyozi, unaingia mle ndani, unakilipia.

62 Halafu kuna magari makubwa. Inatubidi kuendesha barabarani, kule. . . Ilikuwa kwamba wangeweza kuendesha . . . Nilipokuja kwa mara ya kwanza kuelekea Pwani ya Magharibi, nilitumia siku kumi na sita katika Muundo wa T, lakini nilifika huku. Sasa, ni yapata siku nne katika Ford. Lakini bila shaka, Ford yangu ya kwanza, na barabara nilizokuwa nazo, ningeweza tu kusafiri maili thelathini kwa saa, na hizo zilikuwa maili kumi na tano upande *huu*, na maili kumi na tano upande *huu*. Lakini tuna barabara kuu sasa, magari makuu, barabara kuu.

63 Nasi, tukijaribu kuwazia, kwa ulimwengu, ya kwamba wana watu wakuu, watu mashuhuri. Wanao kwenye redio na televisheni, *Mtu mkuu*. Wanataka jamii kuu. Hitler alisema Wajerumani ni jamii kuu, Stalin alidhani Urusi ilikuwa ni jamii kuu, Khrushchev anawazia jambo lile lile. Uingereza ilisema, "Maadamu kuna ulimwengu, kutakuwako na Uingereza," jamii kuu. Marekani inafikiri wao ndio jamii kuu, "Tuna akili na kila kitu, hizo tu ndizo tunazohitaji, kwa hiyo sisi ndio jamii kuu."

64 Jamii kuu, njia kuu, kila kitu kikuu, kikuu. Haina budi kuwa kubwa, kubwa kuliko kawaida. Mtu mmoja hana budi kuwa . . . hana budi kuwa na nyumba kuu. Zinabadilika kila mwaka, nyumba za muundo wa 1962 hazitafaa katika 1963. Friji yako haina budi kuwa bora kidogo, haina budi kupiga hatua kidogo. Kuweka tu *pambo* zaidi juu yake, na kukufanya uibadilishe na ile ya zamani, na kulipia kidogo, dola mia tatu zaidi upate nyingine. Hivyo ndivyo ilivyo. Kila kitu ni kikuu. Ni mpango mkubwa tu wa kutafuta pesa. Nafikiri tulikuwa afadhali tukiwa na farasi na mkokoteni. Hiyo ni kweli.

65 Imefikia mahali ambapo, kama nilivyokuwa nikihubiri hivi majuzi, ni wakati wa kulipuka, kila kitu kinalipuka. Watu wanalipuka, wanajijengea presha nyingi kupita kiasi. Kwa nini usipunguze mwendo upate kuishi? Huh? Hiyo ni kweli. Mbona una haraka hivi? Hatuna budi kuwa na mikutano mikuu kanisani mwetu, dakika kumi na tano. Sasa, huo ndio mtindo wa kisasa, kama dakika kumi na tano, ama usininii, halmashauri ya mashemasi inakupeleka huko nyuma na kutaka kujua kuna nini.

66 Kwa hiyo ni, kila kitu ni kikuu. Yote haya ni ishara zinazoelekeza kwenye giza linalokuja, hiyo ni kweli, kufikia wakati usiojulikana. Tunaingia katika wakati wa fumbo, usiojulikana ambapo mambo makuu yatatokea katika imani ya tafakuri. Hawajui wanakoelekea.

67 Mtu ataendesha gari barabarani kwa mwendo wa maili tisini kwa saa, ahatarishe kuvunja shingo yake, na familia ya mtu mwingine iuawe, asimame kwenye kilabu ya pombe, anywe kwa saa mbili kabla hajaenda nyumbani. Kwani ana shida gani? Zote ni harakati za kuharakisha mambo kupita kiasi, ingekuwa afadhali kama tungechukua tu muda wetu.

68 Sasa, mwanadamu daima amejaribu nafsini mwake kufanya jambo fulani kujitengenezea mwenyewe kumbukumbu. Tumekuwa na baadhi ya hayo yakitendeka hivi punde, kama sote tujuavyo. Lakini ni wazo tu kwamba mwanadamu anataka kufanya jambo fulani kwa ajili ya mafanikio yake mwenyewe, hataacha mambo jinsi yalivyo, hana budi kuyafanyia jambo fulani.

69 Katika nchi yetu iliwabidi kukata misitu yote, na hiyo inaacha dhoruba zipite na kurarua kila kitu. Na sasa, waliufunga mto, ambao hufanya mafuriko yafurike na kufagilia mbali miji. Sasa, wana mabomu mengi sana makubwa na kadhalika mpaka mabango ya "Cheche za mnururisho," "Hatari" yako kila mahali. Urusi imeyaachilia huko, miaka michache sasa na bahari itaanza kuchemka, na—nasi sote tutauawa na cheche za mnururisho, wanasema.

70 Watu wana shida gani hata hivyo? Anajaribu kufanikisha jambo fulani mwenyewe. Hiyo ni ninii yake. . .Kwa nini? Ameumbwa hivyo, lakini, kitu fulani ndani yake kilifanya hivyo, bali yeye hakichukui kwa njia nzuri, anajaribu kulichukua kwa mafanikio yake mwenyewe.

71 Adamu, mwenyewe, alijaribu kuunda dini kuu bila ya upatanisho. Adamu alitaka kuunda dini ambapo angeweza kuishi tu vyovyote utakavyo, kuvaa nguo ndogo ya majani ya mtini, na ni hayo tu. Mnaona?

72 Kaini alijaribu jambo lile lile, badala ya kuleta damu, ule upatanisho, alileta matofaa, mapera, ama matunda yoyote yale ya nchi, akijaribu kuunda kitu fulani mwenyewe, akijaribu kufanikisha jambo fulani.

73 Nimrodi alijaribu kujenga mnara mkubwa mno, mkubwa kuliko minara mingine yote ulimwenguni ili aweze kupanda juu kama, kama Mungu akimkasirikia, mbona angepanda juu ya mnara nayo mafuriko yangepita chini yake, mnara mkubwa mno.

74 Nebukadreza alijenga jiji kuu sana, lilikuwa na bustani zinazoning'inia, na palikuwa ni mahali pazuri sana, palifananishwa na Mbinguni. Papo hapo mbele ya kile kiti cha enzi ulitiririka mto Frati, nao waliona ya kwamba hivyo ndivyo Kiti cha Enzi cha Mungu, ule mto wa Uzima karibu na Kiti cha Enzi cha Mungu, ulivyo.

75 Kujaribu kufanikisha jambo fulani, kujaribu kulifanya kubwa, kuu hivi kwamba angeweza, "Angalia—angalia yale niliyofanya!" Ukuu, uko tu ndani ya mwanadamu.

76 Taifa letu lenyewe, liliionea Uingereza wivu, si muda mrefu uliopita, likajenga meli kubwa mno, wakasema isingeweza kuzamishwa, bali ilizama, Titaniki, meli kubwa mno. Walisema, "Haiwezi kuzamishwa." Lakini ilizama hata hivyo. Ndipo mshairi akaandika ule wimbo, "Mungu, kwa mkono wenye nguvu, anaonyesha ulimwengu huu hauwezi kusimama." Hiyo ni kweli.

77 Ufaransa ilijenga ngome kuu ya Siegfried, waliwazia, "Tutajenga ngome hii, nyuma yake tunaweza kuwa pamoja na wanawake, pesa, na divai, na chochote tutakacho. Na kama Ujerumani ikipata kutufuatilia, jambo pekee tutakalofanya, tutawashambulia tu kwa bunduki hizi na kuwarudisha nyuma," ile ngome ya Siegfried. Lakini ilikuwaje? Walisahau jambo fulani. Ujerumani ilizunguka nyuma yake, wasingeweza kuzigeuza zile bunduki, wakaiteka.

78 Ujerumani ikajenga ngome ya Maginot, ngome kubwa ya Maginot, wakajiimarisha mle chini, lakini moja kwa moja wakaja Wamarekani na kombora angamizi na kuilipua. Mnaona, wakijaribu kufanikisha jambo fulani wao wenyewe.

79 Kanisa limejaribu kufanikisha dhehebu kuu. Hiyo ni kweli. Tumeulizwa magazetini hivi majuzi, mmekuwa mkiliona, "Kwa nini makanisa yote yasiungane yakawa moja na kurudi kwenye kanisa mama, mahali lilipoanzia, huko Rumi?" Ninataka mwanachuoni mmoja, nataka mwanahistoria mmoja, nasi tuna mmoja wa walio bora sana ameketi papa hapa, ninataka msomi mmoja, mhudumu mmoja, mwanahistoria mmoja anionyeshe ambapo Kanisa lilianzia Rumi. Kanisa lilianzia Yerusalemu kwenye Siku ya Pentekoste. Hiyo ni kweli.

80 Mimi, nitamwamini papa, kama anataka kulirudisha kwenye *Hilo*, nitaambatana naye *Huko* nyuma, hiyo ni kweli, bali si Rumi. Nitakubali hili: Rumi ni mahali mama pa dini yote ya kimadhehebu, nayo Biblia ilisema katika mlango wa 17 ya kwamba alikuwa ndiye, naye alikuwa na binti zake nyuma yake.

81 Lakini kila mmoja anajaribu kujenga dhehebu kuu. Ni vibaya sana linaingia kwenye yetu, pia. Ili kupata washiriki tunaongoa, na kuvuta, na chochote kile tupate washirika, tukijaribu kuunda dhehebu kubwa mno, na halafu, wanapopata dhehebu kubwa, wanajaribu kulifanya kuu sana kwa kumleta meya wa jiji, na hakimu, na waliovalia nadhifu zaidi, na wenye elimu bora zaidi. Unapata tu kundi la kielimu la upuuzi baridi, usio wa kawaida. Hiyo ni kweli.

82 Inanikumbusha tu, majira ya kuchipua yamefika hivi punde nami ninawaangalia ndege wakijenga viota vyao. Nami namwazia maskini mama ndege, anaweza kujenga kiota chake,

na kupanda juu yake, atage mayai yake, lakini kama maskini mama ndege huyo hajakuwa pamoja na ndege wa kiume, kamwe hayataanguliwa. Hayo mayai, haidhuru anayatunza jinsi gani, jinsi alivyo mwaminifu, anavyoyafunika kwa mabawa yake, anayageuzageuza, anafanya yote awezayo, na kuketi pale mpaka anajinyima chakula, hayo mayai kamwe hayataanguliwa kama hajawahi kuwa pamoja na ndege wa kiume, maana hayajarutubishwa.

83 Hivyo ndivyo ilivyo na dini yetu ya kimadhehebu. Mradi tu tunawachukua hao wenye dhambi kama washiriki tu wa kanisa letu, mnaweza kuwabembeleza na kuwafanya mashemasi, huku wameoa mara nne ama tano, na kuvuta sigara, na kunywa pombe, na kucheza kamari, na kudanganya, na kusema uongo, na kuwafanya hao mashemasi kanisani, unaweza kuwazunguka-zunguka, na kufanya lolote utakalo, mpaka watakapokutana na yule Mwenzi, Kristo Yesu, hao ni kundi la mayai yaliyooza, kitu hicho chote kinahitaji kutupwa nje ya kiota, kamwe hayataanguliwa. Jambo bora zaidi la kufanya ni kusafisha hicho kiota, kuanza tena.

84 Kutana na yule Mwenzi, Kristo Yesu, ndipo hakutakuwako na tofauti nyingi sana, madhehebu makubwa mno, yaliyo makuu sana, "Sisi ni wafuasi wa *Ninii*, dhehebu *hili*. Sisi ndio wakuu kuliko wote miongoni mwao. Sisi ni wafuasi wa *hili*."

85 Sasa, wanawaomba myaunganishe, myafanye yote kitu kimoja; itafanyika, itatendeka. Hivyo ndivyo watu wanavyotaka, jambo kuu, kila mtu kusema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa *fulani-fulani*, ndilo kubwa kuliko yote ulimwenguni, dhehebu kubwa kuliko yote." Hakika. Wanapenda hilo, maana ni kuu.

86 Mambo haya yote yalishindwa, Titaniki ikazama, ngome ya Maginot ikalipuliwa, mnara wa Nimrodi ukaporomoka, Babeli ilianguka, nayo madhehebu yakafa, ni historia, mavumbi. Haleluya!

87 Daima wametaka ishara. Mungu akasema, "Nitawapa moja." Ndugu, ile—ile radi iliyogawanyika katika anga nyeusi usiku inaonyesha ya kwamba kunaweza kuwa na nuru wakati wa giza. Mungu alisema, "Nitawapa ishara, sio mnara uliopambwa vizuri, sio mnara wa kikanisa, nitawapa ishara, nayo itakuwa ni ishara ya milele, ishara ya Milele, moja ambayo haitakubidi kuendelea kuijenga. Itakuwa ni ya ishara ya milele, ishara kuu, bikira atachukua mimba." Loo, jamani!

88 Ngome zao zote kubwa zilizopigwa msasa, na shule, na—na majeshi, na meli, na chochote kile, bali Mungu alisema, "Nitawapa ishara, na itakuwa ni ishara kuu, ishara ya Milele, ishara ya dawamu, bikira atachukua mimba." Amina.

89 Ni kitu gani? Ya kimbinguni. Ni ishara kuu, si kitu kilichopigwa msasa, bali ni ishara kuu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, maskini Yehova aliyezaliwa katika hori juu ya

lundo la samadi, maskini Yehova akilia kama mtoto maskini, maskini Yehova akicheza mitaani, bali ni ishara kuu. Amina. Ingawa inazungumziwa, hata hivyo ni ishara kuu ya Mungu, ishara ya Milele.

90 Hakuja pamoja na salamu za Mbinguni: Mungu alishusha ushoroba, nayo majeshi ya Malaika yakashukia kwenye ngazi hadi kwenye uwanja wa Kayafa, nao wote wakacheza bendi, na Malaika wakacheza kote duniani; alikuja kupitia ghalani, zizi, bali ilikuwa ni ishara.

91 Si kila mtu aliyeiona, bali wale waliochaguliwa kuiona waliiona, Mungu huonyesha ishara Zake kuu kwa wale waliozaliwa kuziona. Hawakuiona, maelfu walioishi katika siku za Yesu kamwe hawakusikia habari Zake, makumi ya maelfu, mamilioni, ambao hawakujua lolote kumhusu Yeye.

92 Yeye hakuja kama njia ya Malaika wakati aliposhuka kutoka Mbinguni. Angeweza kuja kama Malaika, alitoka Mbinguni, angeweza kuja kama Malaika, angeweza kuja kama kerubi, lakini badala yake, Yeye alikuja kama uzao wa Ibrahimu, Mwanadamu, Mungu akijifanya Mwenyewe Mwanadamu kusudi aweze kufa. Asingeweza kufa katika Roho, ilibidi afanyike mwili kabla hajafa; bali ilikuwa ni ishara kuu, ishara maalum.

93 Yeye alikuja apate kuwa Uzao wa Ibrahimu, apate kuonyesha jamii kuu. Sasa, Ibrahimu alikuwa na uzao, uzao wa kawaida, kisha akawa na Uzao mkuu. Mungu amejaa mambo makuu pia, kumbukeni. Naye Ibrahimu alikuwa na Uzao mkuu, Naye Yesu alikuja ili aweze kukomboa Uzao mkuu wa jamii ya Ibrahimu, Mungu alikuwa na hakika ya kufanya jambo hilo, kupiga mbio pamoja na ishara za kimbinguni za Kristo wa kimbinguni.

94 Baada ya miaka elfu mbili ya kujaribu sana, pamoja na makambora yao yote, na makorongo ya barafu, na chochote kile, wao. . . vipindi vyao vya kuganda, na madhehebu yao kamwe hayajaweza kugandisha, kusukuma nje, wala kuharibu Ishara kuu ya Mungu, Yu hai leo baada ya miaka elfu mbili, Yeye ndiye Ishara kuu ya Mungu.

95 Huenda ukabomoa mnara, huenda ukazamisha mji, huenda ukazamisha meli bali huwezi kuizamisha ishara kuu ya Milele ya Mungu, ni ishara ya milele. Ufufuo wa Kristo usingeweza kuangamizwa, ile ishara kuu mno ambayo Mungu alitupatia.

96 Tunaona katika Agano la Kale, uzao wa Ibrahimu, kulingana na Mwanzo 22:16 na 17, uzao wa Ibrahimu ulikuwa umiliki malango ya adui yao. Mungu aliahidi hilo mlimani wakati Ibrahimu alipoliita Jina Lake Yehova-Yire, "Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu." Mungu atalijalia.

97 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Mwana-kondoo huyo alitoka wapi? Ibrahimu alikuwa kwenye safari ya siku tatu, mtu yeyote wa kawaida anaweza kutembea, loo, maili ishirini na tano

kwa siku, alikuwa safari ya siku tatu kutoka kwenye ustaarabu, kisha akapanda juu ya mlima palipo na wanyama wakali, hakuna maji, hakuna chakula, na huko juu ya mlima, naye akatoa, akaanza kumtoa mwanawe mwenyewe kwa agizo kutoka kwa Mungu, basi alipoanza kuutoa uhai wa huyo mvulana, kondoo dume alilia nyuma yake. Huyo kondoo dume alitoka wapi?

98 Sasa, halikuwa ni ono, yeye alimwua, damu ikamtoka. Halikuwa ni ono, ilikuwa ni kondoo dume. Ndipo Ibrahimu akamwita, *Yehova-Yire*, "Bwana anaweza kujipatia Mwenyewe dhabihu." Ishara kuu, ya kimbinguni. Nao uzao wote wa kawaida wa Ibrahimu kupitia kwa Isaka ulimiliki kila mlango wa adui waliyemfikia. Hiyo ni kweli kabisa.

99 Nina mstari wake ulioandikwa hapa chini, imetuchukua alasiri nzima kumaliza. Vipi kuhusu hebu tuzungumze kwanza, kwa muda kidogo tu, kuhusu wale wana wa Kiebrania, wakati walipoingia katika ile tanuru ya moto? Sasa, hawakuwa na hakikisho lolote, ila tu kwamba walikuwa ni uzao wa Ibrahimu. Mungu hakuwaambia lolote, wala Mungu kamwe hakuwaambia, "Sasa, ninyi shukeni mwende kule, na mwingie katika moto huo, nami nitakuwa karibu nanyi." Lakini walikuwa ni uzao wa Ibrahimu, nao walijua walikuwa na haki, ndipo wakasema, "Hatutalighairi Neno la Mungu. Mungu alitwambia tusizisujudie sanamu, Naye anaweza kutukomboa, asipofanya hivyo, hatutaisujudia sanamu yako." Nao wakamiliki lango la tanuru ya Babeli, lango la moto, walimiliki.

100 Danieli alimmiliki adui wa simba, lango. Musa alimiliki Bahari ya Shamu, kisha akammiliki adui huko Misri. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa ni uzao wa Ibrahimu.

101 Shamgari, jamaa mdogo, mmoja wa waamuzi wa Israeli, ni kifungu kimoja tu kilichoandikwa habari zake katika Biblia. Siku moja alikuwa amesimama kwenye mlango wa ghala lake. Nao Wafilisti wangeingia na kula chakula chao chote, wangefanya kazi kwa bidii majira yote ya kiangazi kisha wapeleke vitu vyao ghalani, ndipo wakaja Wafilisti na kuwanyang'anya.

102 Siku moja labda alikuwa amekusanya chakula chake chote, akamtazama maskini mke wake aliyesimama pale, naye alikuwa mwembamba, na watoto wenye nyuso zilizopauka, akawaangalia maskini jamaa hao wadogo, jinsi walivyokuwa na upungufu wa damu kwa utapiamlo ama kitu fulani, akaona jinsi walivyomwangalia, naye akasema, "Vema, labda msimu huu wa baridi kali tunaweza kupata chakula. Labda ninaweza kuuza ngano kidogo, na kukununulia nguo ya msichana huyo mdogo, viatu vya mvulana huyo mdogo."

103 Hapa akasikia kitu fulani kikija barabarani, hawa hapa Wafilisti elfu moja wanakuja, wenye silaha, mikuki, panga

zinaning'inia ubavuni mwao, watu waliofunzwa, *pump*, *pump*, wakaja moja kwa moja barabarani. Maskini Shamgari akasimama pale, angeweza kufanya nini? Alikuwa mkulima, hakuwa askari, wala hakuwa na kitu cha kupigana nacho, akaangalia, hapo pembeni, na kulikuwa na konzo la ng'ombe. Nanyi mnajua hilo ni nini, na yeyote wenu Wakentaki anapaswa kujua. Unapolima, fimbo unayompiga nao maksai. Kwa hiyo yeye. . .Hilo hapo konzo la maksai limewekwa hapo pembeni, naye akaangalia, hilo. Labda lilikuwa na kipande kidogo cha shaba nchani, ambapo lilichokoa matope kutoka kwenye jembe, na kumpiga maksai walipokuwa wakiendelea. Nao hilo hapo pembeni, akasimama na kuangalia, huku wakipanda kuja barabarani.

104 Hakuwa na wakati wa kwenda kujifunza jinsi ya kupigana, mwajua, na jinsi ya kutumia konzo la—lake la maksai ama upanga. Lakini alikumbuka jambo moja, ninaamini, ya kwamba alikuwa ni Mwisraeli aliyetahiriwa, alikuwa ni uzao wa Ibrahimu, alikuwa na haki kwa ahadi ya kwamba angemiliki mlango wa adui yeyote. Amina. Pande zote mbili, Yeye alimwambia Rebeka jambo lile lile, na Ibrahimu jambo lile lile.

105 Huyo hapo, uzao wa hao mume na mke, naye alikuwa na haki kwake, kwa kuwa alikuwa ametahiriwa, alikuwa ni—alikuwa ni Mwisraeli, alikuwa ni uzao wa Ibrahimu, alikuwa na ahadi ya Mungu kwamba angeweza kumiliki mlango wowote wa adui yeyote. Haleluya! Roho wa Mungu akaja juu yake, naye akachukua konzo hilo la maksai na kuwaua hao Wafilisti elfu moja. Naam. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa na nguvu kuu.

106 Samsoni alikuwa na nguvu kuu, kwa sababu Roho mkuu alikuja juu yake, hiyo ndiyo sababu mfupa wa taya haukuvunjika, tulikuwa tukizungumza habari zake jana usiku, zilikuwa nyingi sana. Hiyo ni kweli kabisa. Hao wote walikuwa uzao wa kawaida wa Ibrahimu.

107 Lakini akaja Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Sasa, Ibrahimu alimpokea Isaka kama mtu kutoka kwa wafu kwa mkewe kwa kujuana kimwili. Sasa, huyo alikuwa kama aliyekufa, huyo alikuwa ni uzao wa kawaida, bali ilikuwa ikielekeza kwenye Uzao mkuu ujao, Yule ambaye hata asingekuwa na baba wa duniani, na wala hakuwa na mama wa duniani.

108 Hilo lilimgusa mtu fulani. Vema, ewe rafiki Mkatoliki, kama unamwita "Mama wa Mungu," Nataka unionyeshe Andiko moja ambapo yeye alikuwa mama yeyote wa Mungu. Mungu angewezaje kuwa na mama? Basi baba alikuwa ni nani? Mariamu hakuwa kitu ila kiangulio, hivyo tu. Yesu kamwe hakumwita hata wakati mmoja "mama," Alimwita "mwanamke," kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu, wala asingeweza kumwita "mama." Sawa. Mafundisho haya ya sharti na mapokeo yame—yamewaua watu, alimwita "mwanamke."

109 Siku moja walisema, “Mama yako anakungojea.” Akawaangalia wanafunzi Wake, akasema, “Mama Yangu ni nani? Hao wafanyao mapenzi ya Baba Yangu.” Alikuwa ni mwanamke tu ambaye Mungu alimtumia, si “Mama wa Mungu,” rehema, la, huko ni kukufuru hata kuliwazia jambo kama hilo.

110 Sasa, Uzao huu mkuu ulikuja. Baadhi yao wakasema, “Vema, sasa, ngoja kidogo, chembe hai, bila shaka, inatoka kwa jinsia ya kiume, ambayo iliumbwa na Mungu, bali lile—lile yai katika huyo mwanamke lilikuwa ni mwili Wake.” Ati lilikuwa? Unafikiri kwamba, kwamba huyo angekuwa huyo mwanamke? Kama ilikuwa hivyo, angalia yale unayomweka Yehova kufanya. Hilo yai haliwezi kuwa hapo bila msisimko, ilibidi jambo fulani litukie, basi angalia mahali ambapo ungemweka Yehova, kumchanganyisha katika kujuana kimwili. Mungu aliumba Utu wote wa Kristo katika tumbo la uzazi la Mariamu, naye alikuwa ni mwanamke tu, kiangulio, kilichomzaa Mwana huyu, yeye hakuhusika. Sasa, yeye ni mwanamke tu ambaye Mungu alimtumia.

111 Sasa, Uzao wa Kifalme ulikuja, nao huo Uzao wa Kifalme ilibidi ufe kwa ajili yetu sote. Sasa, kila mmoja wa wazao hawa wa Ibrahimu, katika mambo ya kawaida, alimiliki kila moja ya malango yao. Jinsi tungeweza kupitia na kuwataja dazani kadhaa hapa, ni malango mangapi, adui wa . . . walimmiliki adui wa malango! Lakini hatimaye ilibidi hao mashujaa wote wakuu wafe, lakini baadaye ukaja Uzao wa Kifalme. Amina.

112 Wakati alipokuwa hapa duniani alimiliki lango la magonjwa, akautwaa. Yeye alimiliki lango la kila adui aliyekuja mbele Zake na kuuteka, Naye akafa, naam, kisha akafufuka tena. Naye alikuwa na funguo za Ufalme wa Mungu, za ninii—ninii . . . kuzimu, mauti, na kaburi, alichukua kila kitu. Yeye alikuwa Uzao mkuu, ile Ahadi kuu. Kumbukeni, ni ishara ya milele, Yeye alifufuka katika wafu, hajafa.

113 Meksiko, siku chache zilizopita hapa usiku, nilikuwa nikisimulia juu ya maskini mwanamke huyo ambaye, maskini mama Mkatoliki ambaye, mtoto wake mchanga alifufuliwa katika wafu. Magazeti yakanihoji kesho yake, nao walikuwa wakisema, “Bw. Branham, wewe si . . . wewe ni asiye Mkatoliki, sivyo?”

Nikasema, “La, bwana, mimi ni Mprotestanti.”

Akasema, “Hulipingi kanisa!”

114 Nikasema, “Ninalipinga, sio watu, kanisa, huo mfumo. Mimi kamwe . . . Mungu alikufa kwa ajili ya watu, hiyo ni kweli, lakini si—siwahukumu watu, ni huo mfumo unaowatawala, huo ndio mfumo ninaouhukumu.”

Akasema, “Basi wewe si tu asiye Mkatoliki basi, wewe ni Mprotestanti.”

Nikasema, "Naam."

"Wewe ni wa dhehebu gani?"

Nikasema, "Ningekuwa katika hali mbaya kadiri walivyowahi kuwa, sina." Nikasema, "Nilizaliwa katika Ufalme wa Mungu." Kweli.

Kwa hiyo basi akasema, "Ninii yako...? Unaamini ya kwamba watakatifu wetu wangeweza kuwafufua wafu pia?"

115 Nikasema, "Mimi..." Jamani, kumbuka asili yangu, mimi ni Muairishi, msingi wangu ulikuwa ni Katoliki, nami nikasema, "Ninajua usingeweza kuwa mtakatifu mpaka ukishakufa," yale waliyosema.

Naye akasema, "Vema, huwezi kuwa mtakatifu mpaka umekufa."

116 Nikasema, "Basi Paulo hakuwa mtakatifu alipohubiri? Petro, Yakobo, Yohana, hao wengine hawakuwa watakatifu mpaka walipokufa, wakafanywa watakatifu na kanisa fulani la Kirumi? Hmm! Usiniambie hilo."

Akasema, "Una maoni gani juu ya kanisa Katoliki?"

Nikasema, "Nasikitika uliniuliza hilo." Naye akasema... Nikasema, "Je, inanibidi kukujibu?"

Akasema, "Ningependa kukusikia."

Nikasema, "Sio kukudharau, bali nafikiri ndiyo hali ya juu kuliko zote za ushirikina iliyopo."

Naye akasema, "Unapataje hilo?"

Nikasema, "Chochote kinachowaombea wafu ni uabudu mizimu."

"Vema," akasema, "unapataje hilo?"

Nikasema, "Miungu hawa wote na miungu wa kike na chochote kile mwombacho, wamekufa."

Naye akasema, "Mbona, Bw. Branham," akasema, "wewe unamwabudu Kristo, Naye alikufa!"

117 Nikasema, "Lakini Yeye alifufuka tena katika siku ya tatu, Naye yu hai sasa." Yeye yu hai milele. Yeye ni ishara kuu. Mbona Yeye? Huwezi kumwua, huwezi kumtia mautini. Amefufuka na yu hai milele, yeye yule jana, leo, na hata milele.

118 Mungu alitupa ishara kuu, ishara kwa ajili ya Neno katika siku za mwisho kwamba Yeye angali hai. Yeye ni... Yeye yu hai (Nini?), leo hii apate kujidhihirisha Mwenyewe kwa Uzao mkuu wa Ibrahimu. Amina.

119 Kumbukeni, Kanisa la Mataifa ni sehemu ya Uzao mkuu wa Ibrahimu kwa sababu Wao wamekufa katika Kristo, na wakawa warithi wa wokovu kupitia kwa Kristo, naye Kristo ni Uzao wa Ibrahimu. Tuna imani ile ile aliyokuwa nayo Ibrahimu. Wakati Mungu alipomwambia Ibrahimu chochote, hakuna dhehebu,

hakuna kitu kingine kingaliweza kukiondoa kwake, aliviita vitu visivyokuwako kana kwamba vilikuwako. Na Uzao wowote mkuu wa Ibrahimu unaamini jambo lile lile, ya kwamba Neno la Mungu ni kweli, haidhuru ni kitu gani kingine kinachotukia. Ninajua hilo linasikika kali, lakini ndivyo ilivyo, ni kweli. Naam, bwana.

120 Isaka alikuwa ni uzao wa kawaida, bila shaka, Kristo ndiye Uzao mkuu. Uzao wa pili ulikuwa ni Kristo, nasi tumezaliwa na Kristo, ambalo linatufanya Uzao mkuu pamoja na Kristo, kwa Mungu. Sasa, sisi ni Uzao mkuu, si shirika, sasa, ama dhehebu. Ni Uzao mkuu.

121 Mungu daima huonyesha ishara Zake, ishara kuu, mambo makuu, kwa watu. Na Yeye—Yeye amefanya, kote katika miaka Yeye daima ameonyesha ishara Zake kwa manabii Wake. Mungu daima aliwafanya manabii kuwa ishara Yake. Ninawatakeni mvae kusikiliza kwenu sasa, maana sina ila kama dakika tano zaidi. Angalieni, Mungu huonyesha ishara Zake, na kila wakati nabii anapojitokeza jukwaani daima ni ishara, kwa kawaida ni ishara ya hukumu ijayo, wakati Mungu anapomwinua nabii.

122 Wakati Mungu alipomwinua Nuhu, ilikuwa ni ishara ya kwamba wakati huo wa kiakili ulikuwa umefikia mwisho wake. Naye Nuhu akahubiri kuja kwa hukumu ya Mungu, naye akakataliwa, na kuchekwa, na kudhihakiwa, lakini Nuhu aliingia ndani ya safina, naye Mungu akawahukumu wale waliomcheka. Nuhu alikuwa ni ishara ya hukumu ijayo, ishara ya Mungu kwa ulimwengu.

123 Musa alikuwa ni ishara kwa Misri ya kwamba Misri ilikuwa imekwisha, Mungu aliwazamisha katika Bahari ya Shamu, wao, walikuwa—waliachwa na yale mapigo. Yeremia alikuwa ni ishara kwa Israeli ya kwamba alikuwa akienda Babeli. Danieli pia alikuwa ni ishara.

124 Yohana Mbatizaji alikuwa ni ishara, baada ya miaka mia nne bila manabii, Yohana Mbatizaji alikuwa ni ishara ya kuja kwa Masihi. Yohana alimtangaza, ya kwamba angekuja. Ndipo basi wakati . . . nini kilichotukia? Jamii ya Wayahudi ilikatiliwa mbali na mti wa wokovu. Naye Yohana alikuwa ndiye tangazo la kuja kwa hukumu.

125 Mungu daima huwatumia manabii kwa ajili ya ishara Zake, sasa, msisahau hilo, mnapomwona nabii akija kwenye wakati. Nami ninaamini ya kwamba tumeahidiwa mmoja, nami ninatazamia hilo. Katika Malaki 4 ilisema . . .

126 Sasa, ninajua mtanikumbusha yale Yesu aliyosema juu yake, "Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye Eliya aliyekuwa aje," ile heri iliyosahauliwa katika Mathayo 11:6. Wakati wanafunzi wa Yohana, baada ya . . . Yohana, kama Eliya, mtu wa mwituni, aliishi mwituni, mchukia wanawake kama Eliya, Eliya aliwahukumu hao wanawake kwa nguvu tu alivyoweza kwa ajili

ya vile walivyokuwa wakiishi, na Yohana alifanya nini? Jambo lile lile, "Si halali kwako kuwa naye," hao wanawake watovu wa uadilifu.

127 Tabia ya nabii huyo, alipenda misitu, na alikaa mwituni, akajitokeza bila woga, aliyapinga madhehebu, akasema, "Enyi kizazi cha nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo? Msiwazie, 'Tunaye *huyu* kwa ninii yetu. . .' kwa kuwa Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Hakuwachezea.

128 Yesu alisema, "Mlitoka kwenda kuona nini? Unyasi unaotikiswa na upepo wowote? Si Yohana, la." Sasa, wakati wanafunzi hawa walipoondoka, Yeye alisema, "Mlitoka kwenda kuona nini?" Akaasema, "Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa habari zake, 'Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.'" Hiyo ni Malaki 3, si Malaki 4.

129 Kwa maana ikiwa hiyo, Yohana wakati huo, basi Maandiko hayajatimia na yalikuwa ya kupotosha, kwa sababu kabla ya kuja kwa ile Siku iliyo kuu ya Bwana, Yeye alikuwa amtume Eliya, na ile Siku kuu ya Bwana itaiteketeza dunia nzima, nao wenye haki watatembea, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, juu ya majivu ya waovu, hiyo isingeweza kuwa kwa Yohana, huyo asingeweza kuwa ni Eliya.

130 Sasa, angalieni, ili kwamba Maandiko yajifasiri Yenyewe kikamilifu. Angalieni, "Naye ataigeuza," Kuja Kwake mara ya kwanza, "mioyo ya baba iwaelekee watoto wao," akiwachukua wale baba zetu wa kale, na kuigeuza imani yao kwenye imani hii mpya ya watoto ya Yesu kuwa. . .akimtangulia, "Ninamtangulia Yesu. Masihi yuaja," akiigeuza mioyo yao iielekee *hii*, kuiondokea torati kwenda kwenye *hii*.

131 Na katika Kuja Kwake mara ya pili, Yeye ataigeuza mioyo ya watoto iwarundie wale baba wa asili wa Kipentekoste tena, hilo linautimiza unabii wa Yoeli ukisema, "Nitarudisha miaka yote iliyoliwa na tunutu, na parare, na kadhalika."

132 Katika bustani ya Edeni kulikuwa na miti miwili, mwanamke mmoja, na Mwanamume mmoja. Wote wanaoishi kwa mwanamke huyo hufa, yeye ni mti wa mauti. Kwa kuwa ulizaliwa na mwanamke, unakufa, unapozaliwa na Mwanamume, Kristo Yesu, unaishi. Angalieni, basi bibi-arusi wa Adamu alitiwa unajisi kabla hajamfikia.

133 Wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuwa ndiye ule Mti wa Uzima, "Mimi ndimi Mkate wa Uzima," Mti wa Uzima, "uliotoka kwa Mungu Mbinguni. Mtu akiula Huu, hafi kamwe."

134 Ndipo alipoondoka, alinunua Mti wa Bibi-arusi. Nao Mti huo uliimarishwa, na kutia mizizi ya nchi kwenye Siku ya Pentekoste. Fundisho lake na kila kitu kilitukia papo hapo mwanzoni, kila kitu ulichohitaji ulipewa papo hapo. Ukakua, nao ukakua kwa yapata miaka mia tatu.

135 Ndipo nzige na tunutu wakaanza kuula, mpaka wakaunyonya uhai kutoka kwake, Nao ukapitia karibu miaka elfu moja ya nyakati za giza. Huyo nzige alifanya nini? Tunutu alifanya nini? Ni mdudu yule yule katika hatua nyingine. Nini kilitukia? Kwanza, ilikuwa ni Wanikolai.

136 Maana, *nikao* maana yake ni "kuwashinda walei," kumtoa Roho Mtakatifu wote kutoka kwa walei, na kumweka juu ya mtu mmoja, askofu, papa, ama chochote kile. Watu mashuhuri wanautaka uwe hivyo, ili kwamba aweze kuwa mbeba dhambi kwa ajili ya wote. Tunaye Mbeba dhambi mmoja, huyo ni Kristo, bali hilo ndilo wanalotaka. Nikolai, *nikao* maana yake ni "kushinda," *walei* ni Kanisa. Kumwondosha Roho Mtakatifu wote. . .Hao si watakatifu, ni mtu mmoja tu mtakatifu. Ni lile wazo la kuingiza pesa kanisani kwa maungamo.

Mtu fulani alisema hivi majuzi, "Je, unaamini katika toharani?"

137 Nikasema, "Naam, bwana." Nikasema, "Si ya aina ile unayomlipa kasisi fulani akuombee. Ninaamini ya kwamba Mungu anazitakasa nafsi zetu sasa hivi, nasi tunapitia wakati wa utakaso, wa kusafisha takataka." Bila shaka.

138 Angalieni, sasa, walimwondosha Roho Mtakatifu wote kutoka kanisani, na kufanya mtu mtakatifu, ule uchaji kutoka kwa kanisa juu ya mtu mtakatifu, wakalishinda. Hilo lilipitia kwenye dhehebu hilo kuu la Ukatoliki lililoitawala dunia kwa mamia na mamia ya miaka.

139 Akatokea mtengenezaji, Luther. Na mara Luther alipokufa, waliliundia dhehebu, ndipo huo mzabibu ukakauka, naye Mwenye shamba akaupogoa. Lilienda wapi? Limekufa. Nionyeshe mahali lilipopata kuinuka baada ya uamsho wa Luther, lilikufa.

140 Kisha akaja, baada ya hapo, John Wesley, hatua ya pili ya huo mti, mtu mashuhuri wa Mungu aliyehubiri Kuhe-. . . Utakaso. Ilikuwaje? Ilikuwaje? Mara Wesley, na—na Asbury na hao wengine walipokufa, waliunda madhehebu na kuunda kanisa kutoka kwake, naye Mungu, yule Mume, akayapogoa matawi nao ukafa; niambie mahali walipowahi kuwa na uamsho mwingine.

141 Ndipo ikaja Pentekoste, pamoja na kurudishwa kwa karama. Ilikuwaje kwake? Nguvu za Mungu zilimwagwa tena, Roho Mtakatifu. Walifanya nini? Wakaliundia madhehebu tena, wakaanza kutenganisha udugu. Basi ilikuwaje? Mungu aliukatilia mbali tu. Hiyo ni kweli.

142 Loo, lakini Mungu kweli alisema, "Nitarudisha, asema Bwana." Huo Uzao, Uhai Wake uko wapi? Moja kwa moja katikati ya mti kuna mkondo wa uhai, si matawi haya yanayoanguka *hivi*, uhai uko moja kwa moja katikati ya mti. Mungu aliahidi haijalishi ni wafyonzaji wangapi

watakaouvamia Huo, kama tunutu wakiula na kuufyonza, na mambo kama hayo, lakini, "Nitarudisha, asema Bwana."

143 Wakati huo Mti unapofikia kileleni, kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa, wakati watu wa Mungu watakapoungana pamoja, ingawa kuna tofauti za madhehebu, basi watakuja kwenye Uzima wa Mungu, na kutakuwako na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ambako kutarudisha tunda la Roho Kanisani tena, itakuwa ni ishara kuu.

144 Sasa, haidhuru kama wewe ni Mmethodisti, hilo ni sawa, Mbaptisti, Mpresbiteri, haidhuru wewe ni wa kanisa gani, hilo halina uhusiano wowote nalo, kama wewe, ukitegemea tu hilo, utakufa, utapogolewa kama tawi lililokufa, wakati huo Mti unapoenda juu. Tunda huenda moja kwa moja juu ya mti, kumbukeni, hapo ndipo jua linapoupiga.

145 Sasa, sasa, jambo ni kwamba, tunapoweza kujileta kwa moyo mmoja, nia moja, mahali pamoja, Mungu mmoja, wokovu mmoja, Roho Mtakatifu mmoja, baraka moja, haleluya, ndipo mtaona ile ishara kuu.

146 Watu wanapoacha kuchanganyikana na agizo hili aliloandika Mungu, wakati watu wanapoacha kuchanganyikana na Biblia, na kurudi na kuliamini Neno, na kulitekeleza na kukaa hapo, sio kwa ajili ya misisimko, bali mpaka Neno Lenyewe litakapohuishwa, na kufanywa Hai, nao waone ishara halisi za Biblia za siku ya mwisho, ile ishara kuu, Masihi yeye yule aliyeishi wakati mmoja . . .

147 Kutatokea nabii moja ya siku hizi, akihubiri Neno asili la Mungu. Unaongea kuhusu mimi kukwambia kuhusu kukata nywele ama chochote kile, ngoja mpaka utakapomshika, ngoja mpaka utakapomsikiliza. Mnafikiri mimi ni mkali kwa madhehebu, ngojeni mpaka atakapotokea, atarudisha miaka yote iliyoliwa na tunutu.

148 Itakuwa ni Ujumbe utakaoenda . . . Baadhi ya watu husema, "Vema, ni dhehebu," nionyeshe wakati mmoja Mungu aliwahi kushughulika kwa njia yoyote ila mtu mmoja, Yeye kamwe hakuwa hata na manabii wawili wakati ule ule, daima ni mtu binafsi.

149 Watu wana mawazo tofauti, yaweke hayo pamoja, unapata mchafuko. Mungu ana mtu mmoja anayefanya kazi naye. Kulikuwako na Eliya mmoja, halafu Elisha, kisha Yohana, na kuendelea hata kufikia Yesu, kadhalika, kuendelea moja kwa moja, kulikuwa na Luther mmoja, Wesley mmoja, na kadhalika, kuendelea moja kwa moja tu.

150 Hapana shaka kutakuja, katika siku hii ya mwisho, kurudishwa kwa Kanisa, Mti huo wa Bibi-arusi, ulioliwa huko nyuma na parare na tunutu, na kila namna ya wadudu wanaokula upendano wote wa ndugu na matunda kutoka Kwake. Hapana budi lije Kanisa tena ambapo mipaka hiyo

itavunjwa, naye Roho Mtakatifu atakuwa na uhuru wa kuingia miongoni mwa watu. Mtakapofanya hivyo, mtaona ishara zile zile na maajabu yaliyotukia huko nyuma katika siku hizo. Amina.

151 Tunaitazamia Ishara kuu, sasa, ile Ishara kuu ilikuwa ni Mtoto aliyezaliwa na bikira ambaye angedumu milele, Ishara ya Milele. Naye Mtoto huyo hajafa. Yeye, walimwua, akafa, bila shaka, ule mwiba wa mauti ulimwua, lakini Mungu alimfufua tena, naye Huyu hapa baada ya miaka elfu mbili ya shida zote, na nzige, na tunutu wakiula. Kungali kuna masalia ya watu wanaomwamini Mungu na kulishika Neno Lake.

152 Na kutakuwako na Bibi-arusi hakika tu kama ninavyosimama katika mimbara hii, kutakuwako na Bibi-arusi ambaye ameoshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo huyo. Naye Mwana-Kondoo huyo atakuwa akiishi miongoni mwao, akionyesha ishara kuu za kufufuka Kwake, baada ya miaka elfu mbili jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani. Ninaamini hilo. Amina.

153 Watu wanataka ishara kuu. Unasema, "Vema, nakwambia, tuna ishara kuu, tuliongeza watu elfu tano kwenye shirika letu mwaka uliopita." Hiyo ni ishara kubwa, hiyo haikuwa ishara kuu ya Mungu, hata hivyo. Ukomunisti uliongeza wengi zaidi ya hao.

154 Jambo lingine, afadhali niseme tu, liko moyoni mwangu, ni kwa nini ninyi watu mnaogopa ukomunisti? Ati mnahofu ukomunisti utautawala ulimwengu? Ninyi watu hamwijui Biblia. Nionyesheni mahali pamoja ambapo ilisema ukomunisti utautawala ulimwengu. Biblia ilisema Rumi itautawala ulimwengu, sio ukomunisti. Loo, ukomunisti ni kibaraka tu mikononi mwa Mungu, ukitumika upate kuwatesa wote kwa jumla na kufanya Maneno Yake yatimie. Jambo lile lile, Yeye alisema, "Ni nani tunayeweza kumtuma kumdanganya Ahabu kumpeleka huko juu, kuufanya unabii wa Eliya utimie?" Ukomunisti hautautawala ulimwengu.

155 Mnaona, Danieli aliona ono hilo, kila moja ya hizo falme zilifuatana, moja kwa moja, na kuendelea, na kamwe halikuingia katika ukomunisti, lilitoka moja kwa moja pamoja na nguvu hizo za Rumi miguuni. Kweli. Urumi utautawala ulimwengu, sio ukomunisti, kwa hiyo usiujali huo, hilo halinisumbui hata kidogo.

156 Jambo linalonisumbua ni kuwaleta watu wangu, hao watakatifu wa thamani wa Mungu huko nje mahali fulani, waanze kuangalia juu *huko*, kuondoa mawazo yako kwenye mambo ya ulimwengu, kupata tukio halisi, ishara hiyo kuu ndani yako, ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, na mambo yote yamekuwa mapya, imani katika Mungu, ishara kuu na maajabu yakitembea pamoja nao, Nuru za jioni. Haleluya! "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Hiyo ni kweli.

157 Ishara kuu: Jua lenyewe litachomoza wakati wa jioni, j-u-a litachomoza, na M-w-a-n-a atatokea, atatokea katika kuonekana Kwake wakati wa jioni. Ni kitu gani? Kuivisha matunda ya Mti wa Jioni. Yeye alisema ataurudisha Mti huo, uliokatwa ukawa Kisiki na ninii. . .namna zote za kanuni za imani, na mafundisho ya sharti, na kila kitu, lakini, "Nitarudisha, asema Bwana." "Nitaurudisha," na itakuwa ni ishara kuu katika Mti huo, kwa sababu Mungu hana ishara nyingine. "Nitawapa ishara ya milele."

158 Sasa, ishara hiyo ilifanya kazi za aina gani wakati alipokuwa hapa duniani? Angalieni yale aliyofanya jana, basi hana budi kufanya vivyo hivyo leo, kwa sababu ni ishara ya milele. Ingawa imenenwa vibaya, ingali ni ishara ya Mungu. "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Tuko katika siku hiyo, marafiki, tuko katika wakati wa jioni, msisahau jambo hilo.

159 Shetani ameyapofusha tu macho ya watu, ameingia makanisani na kuyachafua kabisa, watu wa thamani, watauwa. Jana niliketi kwenye mkahawa, ama, katika—katika m—mkahawa mzuri, huko Los Angeles, ambapo watu fulani wa thamani walinipeleka, kulikuwa na wafanyabiashara, kulikuwa na Waepiskopolia, na kadhalika, wameketi mle, waliojazwa na Roho Mtakatifu. Ni kitu gani? Wameiona Nuru. Mara hiyo Nuru ilipowamulika, walikuwa ni Mbegu, majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Nuru hiyo ya Mungu ilipowaangazia.

160 Mtu mmoja alisema, "Nilifikiri walikuwa wakiwapumbaza akili watu hao," alikuwa kwenye mkutano wa Phoenix, "lakini," kasema, "nilipoona kwamba upumbazaji akili hauwezi kushuka na kuyatambua mawazo ya moyo wa mwanadamu, nikaona kwamba upumbazaji akili hauwezi kufanya mambo haya, nami nikaambatana nao, wao si wasomi," akasema, "wao si watu wenye elimu, ni wanyenyekevu wawezavyo kuwa, wanafungua tu moyo wao," akasema, "huyo ni Mungu, nami ninamtaka," akaanza kunena kwa lugha papo hapo. Amina.

161 "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Ile Ishara kuu itajionyesha kote kwenye Nuru ya jioni. Kumbukeni, jua lile lile linalotoa nuru jioni ndilo jua lile lile linalotoa nuru asubuhi; si aina tofauti ya nuru, ni nuru ile ile. Mnalipata?

162 Mungu alisema, "Nitawapa Ishara ya Milele, nayo itakuwa ni Mwana." Naye huyo Mwana, wakati alipowaangazia watu wa mashariki, sasa anawaangazia watu wa magharibi. Sasa, huwezi kwenda mbali zaidi, jua husafiri kutoka mashariki hadi magharibi, kama vile ustaarabu ulivyosafiri, tuko kwenye Pwani ya Magharibi, tukienda mbali zaidi, tumerudi mashariki tena. Ni wakati wa mwisho.

163 Kristo wa thamani, Mungu wa Milele, anajiangaza Mwenyewe juu yetu, akijitambulisha Mwenyewe ndani yetu. Kwa kitu gani? Akiwakilisha Neno Lake kwa Utimilifu na kwa Neno. "Basi itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili," ishara kuu, ishara kuu.

164 Tunapata ishara kuu. Tumekuwa na ishara za kimadhehebu, tumekuwa na ishara za kanuni za imani, ishara za mafundisho ya sharti, na kadhalika, lakini sasa tunapata ishara kuu, Mwana wa Mungu, akidhihirishwa ndani yetu katika Utu wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Mungu ndani yako, Mungu akitenda kazi katika mwili wa mwanadamu, huo ni Uzao wa Ibrahimu.

165 Angalieni, mwishoni, kabla tu Ibrahimu hajatenganishwa na Lutu, na Sodoma kuteketezwa, Mungu alishuka katika mfano wa mwanadamu, Naye akala. Mhudumu mmoja aliniambia, si muda mrefu uliopita, akasema, "Ndugu Branham, sasa una busara sana kwa hilo."

Nikasema, "La, sina, sina busara sana." Nikasema, "Hilo—hilo linaonyesha tu nina akili timamu."

Akasema, "Unaamini huyo alikuwa ni Mungu?"

Nikasema, "Ibrahimu alimwita Mungu." Nikasema . . .

Akasema, "Huku akila nyama hiyo na kula mkate huo na kadhalika?"

Nikasema, "Naam." Nikasema, "Unasahau tu jinsi Mungu alivyo mkuu."

166 Ninaamini hao walikuwa ni Malaika wawili. Sasa, mnaona, tumeumbwa tu kwa elementi kumi na sita za dunia, hiyo ni kusema, mwajua, kalisi, potashi, petroli, nurulimwengu, na kadhalika, Mungu alinyoosha tu mkono na kuchukua konzi la vitu hivyo, na kufanya *Whiu*, kasema, "Ingia humu ndani, Gabrieli, tunaenda chini," Naye kajifanyia Mwenyewe mmoja. Hiyo ni kweli.

167 Loo, nina furaha sana kumjua namna hiyo! Ingawa huenda kusiwe hata na chembe moja yangu iliyosalia duniani, lakini Mungu wangu, aliyeahidi kunifufua katika siku za mwisho, anaweza kunena, nurulimwengu na kadhalika zitakuwepo, mradi tu jina langu liko kwenye Kitabu Chake, amina, limeandikwa mle kwa Damu ya Mwana-Kondoo. Ishara kuu.

168 Hivi hamna furaha? Hivi hamumpendi tu kwa moyo wenu wote? Yeye ni mwema sana. Ninampenda kwa yote yaliyo ndani yangu. Mungu na adhihirishwe. Amina. Ninaamini ya kwamba Yeye yupo hapa. Amina. Jambo fulani lilitukia tu wakati uo huo, niliona jambo fulani likitukia. Amina. Yeye daima huliunga mkono Neno Lake kama ni kweli, ishara kuu. Angalieni hili:

169 Pale pale, kuna mtu pale kutoka ng'ambo ya bahari. Hebu mfasirie. Unatoka Denmark, unaugua, tatizo lako liko kwenye

mishipa yako, kwenye misuli yako. Mwambie, "Sahau hilo, rudi kule ukawe mzima."

170 Ishara kuu! Mnaiamini? Ishara kuu. Ninyi watu mnaonaje? Mnaamini? Mwaminini Mungu, msiwe na shaka.

171 Huyu hapa ameketi mtu hapa anayejiandaa kufanyiwa upasuaji, ana uvimbe. Bw. Harrison, kama ukiamini kwa moyo wako wote, haitakubidi kufanyiwa huo. Kama utaamini Neno la Mungu na kumwamini Yeye, yote yatakwisha. Ni juu yako, kama unataka kumwamini au la.

172 Mama kutoka Sacramento aliyeketi pale mwenye ugonjwa wa matumbo, je, unataka kuamini kwa moyo wako wote? Mungu atakuponya. Unaweza kuupokea wako.

Ishara kuu!

173 Na wewe je, Bw. Love? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa afya? Vema. Simama kwa miguu yako na upokee.

Simjui mtu huyo, sijawahi kumwona.

174 Ugonjwa wa kibofu, shinikizo kuu la damu, ugonjwa wa tezi dume. Hebu nikwambie jambo lingine, unamwombea mtu mwingine, ni mke wako, hayupo hapa. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Kama nikikwambia mke wako ana shida gani, utaamini uponyaji wake? Ana shinikizo kuu la damu pia, amini sasa, naye atapona.

Ishara kuu.

175 Weka mkono wako juu ya mtu huyo anayeketi karibu nawe hapo. Huna kadi ya maombi, sivyo, Bwana? Vema, amini kwa moyo wako wote nao ugonjwa huo wa mgongo utakuacha.

176 Vema, Bwana, kwa kuwa ulinyoosha mkono, ukitaka kumsaidia pale kidogo, weka mikono yako juu yake. Kama utaamini, hiyo lukemia itakuacha, nawe utapata afya, amina, kama utaamini kwa moyo wako wote.

177 Mwaminini Mungu. Ishara kuu, ishara ambayo haiwezi kushindwa, Mungu wa Mbinguni amesimama hapa. Aliahidi angefanya hivyo, sivyo? Unaamini kwa moyo wako wote?

178 Sasa, hebu niwaambieni, chochote nje ya kuzaliwa mara ya pili hakitaufikia Unyakuo. Isipokuwa kuwe na Chembe ya Uzima ndani yako, utaangamia, huwezi kufufuka tena. Kama huna Chembe hiyo ya Uzima ndani yako alasiri ya leo, na wewe si Mkristo, kwa nini usije moja kwa moja hapa, upitie hapa, na uniache niombe pamoja nawe? Mtafanya hivyo? Simameni.

179 Siamini katika huruma hizi zote hapa. Huendi Mbinguni kwa mihemuko, unaenda Mbinguni kwa sababu unaamini Neno la Mungu, utamkubali Yesu Kristo, hilo ndilo.

180 Kama kweli huna Mungu, njoo papa hapa. Ni—ninajisikia tu kuongozwa kufanya jambo hili, kuacha kuwaombea wagonjwa.

Ninamwomba mtu yeyote asiye na Mungu, asiye na tumaini alasiri hii ya ufufuo, ishara kuu ya Mungu ikitenda kazi miongoni mwa watu, njoo sasa hivi na uamini kwa moyo wako wote.

181 Mungu akubariki, Bwana. Mtu mwingine amfuate. Endeleeni tu kuja, endeleeni kusimama na kuja. Vema, Kijana Mwanamume. Hiyo ni kweli, Bwana, shuka uje moja kwa moja. Amina. Njoo moja kwa moja humu ndani. [Ndugu Branham anaondoka kwenye maikrofoni kuwaombea watu, mengi ya maneno hayatambuliki—Mh.] . . .?. . .

182 Hiyo ni kweli. Jifanyieni tu mstari mdogo hapa. Zungukeni moja kwa moja, mpige magoti karibu na viti. Tutawaombea hivi punde. [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea watu, mengi ya maneno hayatambuliki—Mh.] . . .?. . .

183 Msirudi kwenye viti vyenu. Rudini moja kwa moja hapa, sisi si . . . [Ndugu Branham anaendelea kuomba kwa dakika tano hivi, maneno mengi hayatambuliki—Mh.] . . .?. . .

Bwana, jalia upako wa Roho Mtakatifu juu ya mwanamke huyu akienda kuwa mmishenari kwa Wayahudi, katika Jina la Yesu . . .?. . .

184 Mtu anayetumia mikongojo anataka kuokolewa, hilo si ni zuri sana? Hivi majuzi kulikuwa na, usiku wa kwanza hapa, kulikuwa na mwanamke mwenye umri wa kama miaka sabini aliyekuja hapa, wala hakuwa amewahi kuokoka. Alimpa Kristo maisha yake, akaenda nyumbani akafa. Kama hiyo si neema, sijui. Kuokoka sasa . . .?. . . Mungu na amjalie ndugu yetu jambo lilo hilo, kabla hajatoka kwenye chumba kile pale . . .?. . . akija na mkongojo wake, amelala upande wa ndani . . .?. . . Mungu ambariki, na ampe Uzima wa Milele, na kuuponya mwili wake . . .?. . . [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea watu, mengi ya maneno hayatambuliki—Mh.]

185 Baba wa huyo msichana mdogo yupo hapa, Myahudi, amekuja na kusema anamwamini Bwana Yesu Kristo . . .?. . . na kumiliki lango la kila adui anayemsumbua, katika Jina la Yesu Kristo. Baraka juu yako, Bwana. Nitakutana nawe Utukufuni kama si kabla ya . . .?. . . [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea watu, mengi ya maneno hayatambuliki—Mh.]

186 (Una mahali pa kinasa sauti?) Sasa, ni wangapi walio na kadi za maombi? Vema, tulianzia wapi usiku uliopita, ama, tuliopoachia? Si ilikuwa ni kama ishirini? Tulikuwa katika gani? I, sivyo? I, ishirini iko hapa? Hapo ndipo tulipoachia, I, ishirini. Ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano, katika I. Vema.

187 Sasa, mabawabu watawasaidia hapa kuingia mstarini. Ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini-. . . I zote. Katika I, mlete huyo. Kadi ya maombi I, ishirini hadi mia moja.

188 Inayofuata ni ipi, J? Vema, Bwana. Vema, wakati wanapokuja, tutaomba. . . Hebu tuone, tutawamaliza wote jinsi gani? Vema, ninyi nyote ombeni. . .?. . .

189 Sasa, J, pia. Wote walio na kadi za maombi simameni. Tutafanya jambo tofauti kidogo sasa hivi, na lile ambalo tumekuwa tukifanya. Wote walio na kadi za maombi simameni *hapa*.

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu;
Tu. . .(Sasa, simameni tu papo hapo. . .), amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

190 Sasa, ili kwamba msifikiri ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni wa mwinjilisti peke yake, watu hawa hapa wana haki ya kuwaombea wagonjwa kama mimi, Oral Roberts, ama mtu yeyote, wote ni watumishi wa Kristo.

191 Na sasa, kama tu mtaamini! Ninataka kuweka mikono juu ya kila mtu anayekuja jukwaani, isitoshe, bali nataka ndugu zangu wahudumu wawe pamoja nami, kusaidia kuweka mikono juu ya wagonjwa, kila mmoja wenu, kusudi mpate kuona ya kwamba ni. . .ninii. . .kusanyiko lenu linaweza kuona kwamba kwa sababu tu wewe siye mwinjilisti, hilo halimaanishi Mungu hayuko pamoja nawe, yuko pamoja nawe tu kama mtu yeyote hapa.

192 Na sasa, sasa, kwenu ninyi watu mtakaokuja kwenye mstari wa maombi, kama ukija ukitarajia kuponywa, utaondoka kwenye jukwaa hilo ukiwa mzima. Sasa, vipi. . .? Sasa angalia, usielewe vibaya sasa, afadhali upate jambo hili dhahiri, maana, kama sivyo, utagonga tu ukuta. Lakini kama huninii. . . Ukilipata dhahiri, jambo fulani liko karibu kutukia. Unaona? Na—na—nawapenda, na ni—ninataka kuwasaidia, bali nyinyi ni. . . Sikilizeni yale nitakayosema.

193 Mwanadamu angewezaje kamwe kupambanua mawazo ya watu, na kuangalia kinachotendeka? Sasa, hiyo ni kweli? Kama wao. . .kama hilo lingefanywa katika—katika Sodoma, ingalikuwa imesimama hata leo. Mnaona? Ni kubwa zaidi, hata ni. . .kumekuwa na mengi zaidi yaliyotukia papa hapa kwenye mstari huo kuliko yaliyoandikwa katika Biblia nzima.

194 Katika mkutano huu mengi yamefanywa katika mstari huo wa ishara kuu, ya kufufuka kwa Kristo, na Uwepo Wake, ikionyesha ya kwamba Yeye ni Mungu yeye yule, Yule yule, akiwa na ishara ile ile, akifanya jambo lile lile. Naye alisema, Mwenyewe, "Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe kwanza la kufanya." Hiyo ni kweli?

195 Sasa, kama Yeye alikuwa amesimama hapa, sasa hivi, amevaa suti hii, asingeweza kukuponya isipokuwa ulimwamini. Sasa, Yeye angeweza kukwambia shida yako ilikuwa ni nini, mambo mengi namna hiyo, bali Yeye asingeweza kukuponya, kwa sababu tayari amekuponya. "Kwa kupigwa Kwake sisi tu*li*ponywa." Hiyo ni kweli? Tayari imekwisha, imekwisha kufanywa, kila mtu.

196 Sasa, sikilizeni kwa makini, juma hili nimejaribu kuwafanya muone njia kuu zaidi ya kufanya jambo hilo. Sasa, kulikuwa na Myahudi wakati mmoja aliyesema, "Njoo, uweke mikono Yako juu ya binti yangu, naye ataishi." Hiyo ilikuwa ni desturi ya Kiyahudi, kuwekea mikono. Lakini yule Mrumi, Mmataifa, alisema, "Sistahili Wewe uje chini ya paa langu, nena tu Neno."

197 Basi mnapoliona Neno Lake likidhihirishwa si kwangu tu, bali kwenu ninyi, imani yangu katika karama, imani yenu katika Mungu aliyeituma hiyo karama, na kuiona ikitenda kazi kati yetu, huyo ni Mungu.

198 Laiti ningaliweza kumfikishia hilo kila mmoja wenu. Laiti ningaliweza tu kulifanya kundi hili dogo kuona jambo hilo, kutakuwako na Pentekoste nyingine itakayotukia sasa hivi, kama ningeweza tu kuwafanya mpate kufahamu ni nini hasa.

199 Sasa, hebu nilipitie tena, iweni na kicho sana sasa, angalieni, Mungu aliahidi mambo haya kutukia katika siku za mwisho, haya hapa yanatendeka. Mimi, ndani yangu, mimi ni mjinga, hata sina elimu ya kawaida ya shule, sijui lolote kuhusu mambo haya, Baba wa Mbinguni anajua hivyo ndivyo ilivyo, bali nilipozaliwa ulimwenguni, nilipokuwa mvulana mdogo tu, nimeona maono na imekuwa ni makumi ya maelfu yao, na kila moja ya hayo limekuwa kamilifu. Hakuna jambo moja, kamwe sijabashiri chochote, pasipo kutukia jinsi hasa lilivyosema lingetukia. Mnaona?

200 Sasa, halafu unaketi hapo, na unadai kuwa Mkristo mwenye imani, basi imani yako mwenyewe inaenda kwenye—kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, na kumgusa Kuhani Mkuu, Naye anarudi kupitia karama na kujibu moja kwa moja kuonyesha Yeye ni Mungu yeye yule aliyekuwako, aliye ndani yangu, na ndani yenu, Yeye ni Mungu yeye yule.

201 Sasa, hiyo ni . . . Mmewahi kuona picha yake huko nyuma, labda mnayo? Malaika yuyo huyo, Nuru hiyo mnayoiangalia kwenye hiyo picha (Nitakapokutana nanyi kwenye Kiti cha Hukumu, kumbukeni hii ni kweli.), hayuko futi mbili kutoka mahali ninapotembea hapa sasa hivi. Hiyo ni kweli. Huliamini, anza kuwazia jambo baya kulihusu, uone kama Yeye hatakwambia habari zake. Unaona? Mungu angali ni Mungu, hana budi kuwa ni Mungu, Yeye ni Mungu, daima amekuwa ni Mungu.

202 Na sasa angalia, kama upako huo hapa. . .Sasa, labda ndugu hawafanyi hivyo, lakini hawa ni wahudumu wengine, kuna karama tisa ambazo zimetumwa kwa Kanisa na Mungu. Hiyo ni kweli? Mitume, ambalo linamaanisha "wamishenari," mitume, manabii, hao ni waonaji, na—na waalimu, wachungaji, wainjilisti. Hizo ni karama hizi zote zinazoketi hapa pamoja, sasa si ofisi moja tu, bali afisi hizi zote pamoja, huku Roho Mtakatifu hapa akizidhihirisha.

203 Hawa wachungaji, wamewafundisha njia ya kuishi, mumefuata maagizo yao na kumpokea Roho Mtakatifu. Mnapokea ninii yao. . .Roho Mtakatifu na kupokea wokovu kwa kufuata yale hasa hao walimu waliwaambia mfanye. Sasa, nilikuja na kuwaambia mumwamini Bwana Yesu Kristo, Yeye angejibu, na hili hapa kupitia karama nyingine. Sasa, mnapitia chini ya mkono wa kila moja ya hizo karama. Ninyi, mnawezaje kushindwa? Haliwezi kushindwa. Unapotembea kwenye jukwaa hili, na mtu wa kwanza anaweka mkono wake juu yako, sema, "Asante, Mungu, kwa kuniponya," uondoke hapo ukishangilia.

Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kila mtu.

204 Bwana, mwishoni mwa mkutano huu wa siku tano, ninatambua hapa, leo, uaminifu wa hawa watu. Nami ninatambua ya kwamba zile shamrashamra na msongamano, na mkazo, Shetani angesababisha mchafuko huo miongoni mwao kuwazuia wasiwe na imani, bali tunakuomba Wewe, Bwana, umzuie. Jalia Roho wa Kristo amwondoshe hapa.

205 Pia jalia watu, wanapopitia hapa jukwaani, wakumbuke wanafuata vile hasa Maandiko yalivyosema wafanye, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hakika, kwa ibada tano mfululizo, thibitisho la Uwepo Wako, kwa kunena kwa lugha, kwa kufasiri lugha, kwa kuwaponya watu, kuwatoa kwenye viti vya magurudumu, na kote mahali hapo, na magonjwa, na—na mambo yaliyonenwa na kuambiwa watu, na halafu, kuona nguvu za Mungu zikiwaokoa, wakiona mambo haya yote yakitendeka, hakika, wanaamini.

206 Kufunua mioyo, siri hata iliyo moyoni, na watu wanaowaombea, wapendwa wao na kadhalika. Hakika, wanaweza kuona ni Bwana Yesu mpendwa.

207 Sasa, jalia aje katika uweza Wake, katika nguvu Zake. Ninawabariki ndugu zangu hapa, Bwana, ambao watasimama pamoja nami, hawa wachungaji na waalimu ambao wamenisaidia, waliosimama hapa karibu nami, Mungu wabariki, mikono na miili yao na ihuishwe na Roho Mtakatifu.

208 Na kwa kuwa watu hawa ni wagonjwa, hao—hao ni watoto wa mtu fulani, mama ya mtu fulani, baba ya mtu fulani, mume wa mtu fulani, mke wa mtu fulani, ingeweza kuwa wangu, Ee Mungu, kwa unyofu wenye kilindi, jalia watu hao waelewe kwamba tayari wameponywa, inawabidi tu kukubali jambo hilo.

Tujalie. "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa," na jalia kila mmoja anayepitia kwenye mstari huu alasiri ya leo aponywe, tunapoweka mikono juu yao, katika Jina la Yesu. Amina.

209 Nitawaomba ndugu zangu hapa, ya kwamba mtafanya mstari, moja kwa moja *hapa*. Njoni moja kwa moja hapa jukwaani. Njoni moja kwa moja hapa na mfanye mstari unaoangalia nyuma upande *huu*, ukiangalia nyuma upande *huu*. Hiyo ni kweli, ninyi ndugu wahudumu . . . ?. . . Sasa, sasa, fanyeni mstari mwingine moja kwa moja upande *huu*.

210 Amina. Ni wakati wa matendo sasa. Roho Mtakatifu alijionyesha Mwenyewe kuwa yupo, Neno limejithibitisha Lenyewe, sasa ni wakati wako wa kutenda, huu ndio wakati wako. Ni wangapi wanaoamini? Vema, mnapofuatilia mstari huu alasiri ya leo, piteni mkiamini. Rudi kitini mwako, ukimsifu Mungu. Haidhuru una shida gani, amini kwa vyovyote vile.

211 Kama kuna yeyote aliyelemaa, nafikiri kuna mtu hapa wa ku—kusukuma kiti cha magurudumu, hebu wawasukume moja kwa moja *hapa*, tutashuka hapo chini na kuwaombea, si lazima wawalete jukwaani, tutashuka huko chini. Haitawabidi kuwanyanyua juu, ama chochote kile, waleteni tu papa *hapa*, nasi tutashuka na kuwaombea.

212 Sasa, ni wangapi katika jengo hili ambao ni wazima, ambao wataungana nasi katika maombi?. . .?. . . Sasa, wageukieni wagonjwa, angalieni ni nani atakayekuwa akiwaombea, angalieni kwenye jukwaa hili hapa.

213 Uwepo wa Roho Mtakatifu, ishara kuu! Ishara hii haijawahi kufanywa Kanisani tangu siku za mitume, huyu hapa mwanahistoria amesimama hapa, sasa hivi, haijawahi kufanywa tangu siku za mitume. Kwa nini? Hii ni Nuru ya jioni, Sodoma imetuzunguka kote, ni kwa ajili ya Kanisa lililoitwa litoke.

214 Sasa, hili ndilo jambo ambalo Mungu anawatakeni kufanya: Pitieni hapa, na mara mnapopita, njoni huku imani yenu imeelekezwa kwa Mungu, na kusema, "Ninaliamini sasa hivi, Bwana, na ninalikubali," uondoke moja kwa moja jukwaani, yamekwisha basi.

215 Vema. Sasa, ninataka watu wote katika kusanyiko pia waombe pamoja nasi sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu wakati watu wakipita.

216 (Hebu tuiweke hii hapa kando, kusudi mtu asije akaikanyaga, kama vile *hapa* kando. Sasa, ndugu, mmoja wenu hapa atachukua *hili*. Ndugu Kopp, labda kama utashikilia *hili* ninapowaombea wagonjwa, Ndugu.)

217 Loo, jambo fulani halina budi kutukia, sivyo? Ni wangapi wanaoamini ndivyo? Ninaamini. Sasa, hebu sote na tuinamishe

vichwa vyetu sasa, kwa uchaji, na, tunapoomba, na hebu kusanyiko lianze kupita sasa.

218 Baba yetu wa Mbinguni, mwanamke huyu anajitokeza sasa katika mstari huu mkuu wa maombi, kwa ajili ya alasiri ya leo, yeye anapitia kwanza, mkono baada ya mkono utawekwa juu yake, na wengine, wanapopita, huku maombi yakipaa juu kila mahali.

219 Sasa, Bwana, hii ni. . .Siamini ungeweza kufanya zaidi ya yale ambayo tayari umefanya. Umeonyesha Uwepo Wako, ulilithibitisha Neno Lako, ukafanya mambo haya yote makuu.

Na sasa, Bwana Mungu, na iwe hivyo, jalia kila mmoja aponywe wanapopitia hapa. Katika Jina la Yesu Kristo, tujalie, Bwana, wanapoenda.

[Ndugu Branham anawaombea wagonjwa, mengi ya maneno hayatambuliki—Mh.]

220 Ninataka kusimamisha mstari kwa dakika moja. Mnamwona maskini mvulana huyu mweusi? Jana usiku aliponywa na kuondolewa huku amepooza, kwenye kiti cha magurudumu, huyu hapa anatembea hapa kumpa Mungu utukufu. . .?. . . Mungu akubariki. . .?. . .

Endeleeni kuomba kila mtu, endeleeni kuomba, mko katika Uwepo wa Mungu.

62-0624 Ishara Kuu
Great Western Exhibit Center
South Gate, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org